**Interjection:** We got the information before the …(inaudible)… no single disabled person here

**Com. Adagala:** Let us just leave it. You don't have the floor, I want to tell you and what am telling you is not anger, it is not kulaumiana ni pain, uchungu. Kila commissioners wametumiwa kwao we go other places the committee is so active, district co-ordinator is so active. Sasa unakuta tu unafika hapa na room umejaa. So, anyway ni mara ya mwisho, pengine iwe na ammendment hii ni mara ya mwisho wacha tuendelee. I would like to inform Juma that we have the draft constitution in braille kwa wale ambao hawawezi kusoma hata mimi nafaa nijifunze braille siku hizi. Sasa tutaendelea, lakini mjue kuna upungufu na tutachukua majina ya wale wamefika hapa kwa kamati wawe ndio watakuwa present. Please write their names down because we cannot go on thinking there is a committee hata tunamtetea kule mimi nikiwa mmoja na chini kazi haiendelei.

Haya katiba, have you viven out copies? How many copies do you give out? Let me see copies of the constitution chairman anayo. Every constituency will receive for now two hundred copies for now. So if you have these thing please let someone else photocopy it, read it go to the district co-ordinator's office to read it. Tumeuliza pesa zetu pia ni pungufu tumeuliza Mr. Lumumba if we can print some more we have asked plenary if we can print some more. So we have there the constitution, lakini zile zilikuja ni za kingereza, haya leo kuna watu kwanza tunafanya hivyo tukijua watu wengi walinunua magazeti. Kwa sababu tukiwa na kitu special hivyo watu hununua magazeti wale ambao wanaweza lakini pia lazima wamesoma na kufikiria.

Hiyo ndiyo njia tungefikia watu wengi na hakuna njia ingine ni ya radio. Watu wangapi walisikiza radio last Sunday? Saa tano

mpaka saa sita kiswahili saa tisa mpaka saa kumi kingereza wangapi. Even when it is on the air, let me tell you watu wanaishi Kenya kama hawana hamu ya kujua vitu. Najua kwa sababu kama baba yetu alipoaga tuliweka kwa magazeti, tutaweka kwa radio, matangazo ikiwa part of news, na still mtu anakwambia sijui. Sasa nashindwa vijana wa Nairobi wanasikiza FM najua kwa FM watu hawafariki kama Kiss FM hakuna mtu anafariki duniani hii ni mbinguni, wanaishi tu kwa maisha yao. Lakini wacheni niwaambie mshughulike, kuna information mshughulike. Haya tutaanza na sehemu gani kijana? Wacha aeleze.

**Vincent Watako:** *Mulembe mwesi.* Sasa mimi ni kijana na mnajua vijana siku hizi hawasikii kimama au hawaongei kimama sana.

**Com. Adagala:** Watasikia

**Watako:** Sasa ningependa kuongea kwa lugha ya kiswahili ndiyo tuelewane vizuri. *Khurechasanie*

**Interjection:** …(inaudible)… sema kwa kiswahili

**Watako:** Sawa nitatumia kiswahili. Katiba wananchi wamepewa kabisa. Mlitaka mpewe fursa ya kutoa maoni na hii katiba nimewapatia fursa mukatoa maoni na maoni yenu yote yameingizwa katika katiba comissioners, wote wametembea sehemu tofauti za nchi hii kusikiza maoni ya kila mwananchi. Sasa nitawaeleza jinsi katiba imekuwa arranged. Kwanza mlitaka katiba ambayo imeandikwa katika lugha ambayo mnaeleza elewa na ninafurahi kuona wazee saa hizi wanasoma na kuelewa. Mnaelewa hiyo katiba muongojee kiswahili inakuja bado inatengenezwa baod mtapata.

**Com. Adagala:** Kingereza inaeleweka. Kuna kingereza cha wakili. Wakili wakienda hata wewe mwingine haujui ni therefore and the whereas natumeandika kwa lugha rahisi ya kawaida. Sio ile kama kabisa standard one lakini ile ambayo mtu ambaye anajua kingereza anaweza kukisooma na pengine akitumia dictionary kwa mambo kadha magumu ataelewa. Lakini ile yetu tunayo sasa ilikuwa ngumu sana tukasema tuweke kwa kiswahili na kingereza. Kwa katiba, sikizeni lugha rasmi ni kiswahili kwanza hii katiba mpya na kingereza. Juu yake, kiswahili kimewekwa lugha ya taifa haiko kwa katiba sasa iko kwa katiba ninaelewa ninawadondolea tu mbele.

**Watako:** Sasa mnaweza kufungua makaratasi ya katiba ambayo mmebeba na inafaa mjue haya ni mapendekezo. Baadaye mtapewa fursa ya kukubaliana nayo ama mseme muongee na wakilishi wenu katika NCC waongeze mabadiliko ua wakubaliane nayo. Lakini kwa ukurasa wa kwanza munaona katiba iko katika milango imegawanyika katika milango/chapters. Sasa katiba yote iko na milango ishirini mnaona, sura.

**Com. Adagala:** Mmeona, imefika mpaka ishirini?

**Interjection:** Ndiyo tumeona

**Watako:** Mmeona, na katiba inaanza na kitangulizi. Sura ya kwanza tunaongea kuhusu nguvu ama sovereignty of the people, nguvu ya watu. Hii ni katiba ambayo imetengenezwa na watu sasa lazima itambue nguvu ya watu. Madam commissioner, ananiambia niseme ni ukubwa wa nguvu ya watu. Sovereignty of the people natumai mmesoma.

**Com. Adagala:** Hebu chapter one …(inaudible)….

**Watako:** Sasa katika sura hii, katiba inawatambua kwamba, matawi ya serikali executive, judiciary na legislature.

**Com. Adagala:** Hiyo utangulizi ni preamble turudi nyuma kidogo au kwa page hiyo. Preamble inazungumzia, maono ya wakenya kuhusu Kenya. Inazungumzia dreams of Kenyans, the aspirations of Kenyans, the vision of Kenyans, how Kenya should be. Tutangulie ndani lakini sasa wacha tupitie tu kwa sura. Lakini preamble inazungunzia ile ndoto, uzuri wenyewe, ile asali yenyewe ungependa Kenya iwe.

**Watako:** Sura ya kwanza inaongea juu ya nguvu ya watu na matawi yote ya serikali, legislature yaani bunge, judiciary-ma-judge na mahakama na executive-rais, prime minister na deputy prime minister wote watapata nguvu zao kutoka kwa watu. Mmesikia.

**Com. Adagala:** Hiyo serikali …(inaudible)… kwa ile nini iko serikali iko tu ndiyo unaona vile unapanga katiba ndiyo maisha yanakuwa, ndiyo umeona hapa mzee akisema serikali inataka tufanye na siyo hivyo sasa ni watu wanataka mahakama na bunge na serikali ifanye, ni watu kutoka chini sio kutoka juu. Nasema hivyo kwa sababu hapa Luyhaland particularly Maragoli tuna serikali kila siku ni serikali sasa bila kusema ya kweli serikali ni watu ndiyo sasa imeingia hivyo lakini kwa ile katiba ingine haikuwa hivyo.

Sehemu hii pia tutakuwa tukizungumza hivyo sehemu hii pia inazungmzia mipaka ya Kenya. Kenya ni nini? Kenya ni wapi? Itakuwa na kitu kinaitwa schedule, kitu kinapangwa, ukurasa mwingine wa nyuma ambayo inaeleza hiyo mipaka ya Kenya watu wamefanya geographia, nafikiri sote tumefanya latitude, longitude inapitia wapi inaenda vipi kwa sababu mipaka yetu hata tunapigania na watu wa Uganda, saa ingine watu wa Sudan sasa hiyo inafaa ipangwe hapo.

**Watako:** Sura hii pia inatambua kwamba jiji kuu litakuwa Nairobi. Lugha za katiba zitakuwa kiswahili na kizungu/kingereza. Pia, katika sura hii dini inatambulika. Siku za holidays, siku ambazo tutakuwa tunasherekea holidays pia ziko katika sura hii. Tunaangalia juu juu sasa halafu sura nne kunazo zile nguzo za katiba ama nguzo ambazo katiba inataka ku-entrench kwa watu. Nguzo hizi ni kama ufisadi, ukome. Katika katiba hii pia, kuna nyinyi kama wananchi mnapewa jukumu la kuilinda katiba, jukumu la kulinda uhuru na nchi yetu iko katika hii sura.

**Com. Adagala:** Hapa tulikuwa na msitu ulikatwa hiyo sasa ni jukumu la kila mwananchi kulinda, sio serikali. Sio unasema serikali halafu unakaa hapo na hauna la kufanya au mto unaharibiwa na huna la kufanya au kitu fulani kwa jamii kinaharibika na wewe huna la kufanya. Wewe kila mwananchi hapa ana jukumu hiyo ana jukumu ya kulinda katiba kila mwananchi anapewa hiyo nguvu na katiba.

**Watako:** Sura ya nne iko inaeleza kuhusu haki za kila Mkenya.

**Com. Adagala:** Kabla hajafika hapa, je Mkenya ni nani? Ni mtu gani anaonekana kama Mkenya. Sasa hapo hilo swali inatokea tujue Mkenya ni nani anatoka wapi anakaa vipi, na nguvu zake haki zake zaidi zinaenda kwa chapter ya tano. Hapo kuna ile inaitwa kwa kiswahili na mkipata ya kiswahili inaitwa ukatiba. Hapa inaitwa bill of rights. Lakini kwa kiswahili walifanya translation waksema hiyo ndiyo inalinda maisha ya wananchi hapo hapo ndiyo mtapata mambo ya elimu, vyakula, kuishi, kushirikiana, jukumu ya wananchi. napitiia juu juu tutapitia tena. Mambo ya haki za binadamu na health education, nimesema hizo, refugees hata wale wakimbizi, soma hiyo yote.

Access to information vile mzee amesema hapa lazima u-demand information. Kutoka sasa uta-demand na lazima muwe munatembelea ofisi ya co-ordinator, to demand the information. Na pia wewe hauna ruhusa ya kutojua hakuna kitu sikujua. Ikiwa watu wetu wanasema *kali kumanyiku mba* nawafikiri ni kitu kizuri. Si kitu kizuri ni aibu sasa hapo pia itakuwa na rights wewe una rights ya information na una responsibility ya kujua. Uhuru wa dini uko hapo. Haya pia unaenda mpaka culture, cultural rights ziko hapo, community, individual rights hizo za mtu binafsi hizo za utamaduni vile mlituambia. Hiyo ya mahakama pia iko hapo mwananchi vile atashiriki kwa nini. Hii chapter six ni representation of the people vile watu watakuwa wakilishwa na hiyo inatokea hapa kwanza.

**Watako:** Katika sura hii kuna haki ya upigaji wa kura pia kuna haki ya registration itakuwa inaendelea throughout. Pia hapa tume ya uchaguzi sasa iko katika katiba yenyewe. Katika sura hii pia kuna vyama vya kisiasa vinalindwa katika katiba vinapewa funds kutoka kwa katiba lakini haitakikani vipate pesa zao kutoka nchi za kigeni.

Katika sura ya saba kuna bunge. Bunge sasa kutakuwa na nyumba mbili ama two houses of parliament. Pia qualifications za kuwa mbunge ziko katika katiba vile uchaguzi wa wabunge utakuwa ukifanywa. Jinsi sheria itapitishwa katika bunge.

**Com. Adagala:** Umefika part four

**Watako:** Sehemu ya nne

**Com. Adagala:** No part four sio sehemu yanne. Sura hiyo, halafu sehemu ya tano ni…

**Watako:** Sehemu ya tano ni kika na calendar ya bunge halafu mambo madogo madogo yaani miscellaneous ndiyo ya mwisho.

**Com. Adagala:** Mulituambia mtaki bunge iwe na tingizo tingizo itafungwa lini itakuwa vipi, itafanywa nini hapo pia iko muhimu na imewekwa kwa katiba. Ikiwekwa kwa katiba hakuna binadamu Kenya hii atapindua.

**Watako:** Sura ya nane nayo inaongea juu ya executive. Viongozi wa executive wote wamepewa mamlaka hapo jinsi watakavyo chaguliwa mamlaka yao na jinsi watakavyotolewa katika ofisi kuna ofisi ya Prime Minister ama waziri mkuu, kuna rais, makamu wa rais. Halafu sura ya tisa ni judiciary and judicial system, mahakama na maofisa wa mahakama. Sura hii inatoa qualifications za judicial officers vile watakavyochaguliwa pia kuna korti mpya zimekuwa introduced katika constitution

tunataangalia baadaye. Mko katika sura ya tisa sasa.

**Interjection:** …(inaudible)…

**Watako:** Utafuata tu, kwa introduction

**Interjection:** …(inaudible)…

**Watako:** Katika katiba hii pia kuna legal system profession. Mawakili na ma-judge pia wamewekwa katika katiba. Sura ya kumi nayo ni devolution of powers. Hii ni kama serikali za wilaya. Sana serikali zitatoka mashambani kwa watu wenyewe.

**Com. Adagala:** Hii devolution of powers ni ile fumbo nilikuwa nimewaambia lilifumbua na likachukua nguvu zote zikawa Nairobi sivyo? Nguvu zote vitu vyote ukitaka kitu kidogo unaenda Nairobi, ukitaka nini all the buses in Kenya go to Nairobi isn't it? Na sasa tunataka vile hi sio kupenda kwetu. Sheria yetu ilituambia angalieni devolution of powers. Nguvu hizi zitakuwa aje? Zitapangwa aje? Ikatuambia tuangalie vile ilikuwa zamani tulikuwa na seminar kuhusu hiyo kati yetu ili tuelewe halafu tukaja hapa na hakuna watu wengi hawakusema devolution of powers. Wale wamepata civic education walisema hivyo lakini wengi walituambia nikitaka cheti cha nini lazima niende Nairobi, kila kitu Nairobi hiyo ni unitary government. Sasa hii ni devolt parliament. *Vinyinyo vyatula.* Sasa hiyo maji itaelekea wapi? *Dukana ganzile ahi gadukana gudahili mkikombe gi ehindi iweko ekindi kii iliati chindi ipeko kijiko inategemea hivyo.* sasa hiyo ndiyo tumefanya na hii chapter iko muhimu sana kwa sababu mbeleni mwaka wa sitini na nne nguvu zilinyakuliwa kutoka kwa wananchi zikaenda centere ikawa unitary government na duniani hatuna unitary government nyingi ni moja, mbili hivi hata hizo zina shida nyingi sana hapa ndiyo tunaweza nani atasimamia hiki na kile na mahakama itakuwa aje. Iko hapo hapa chini mashinani.

**Watako:** Sura inayofuata ni ya kumi na moja ambayo inaongea juu ya mashamba na mali kwa jumla.

**Interjection:** …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Wacha tumalize tutakuwa na nafasi.

**Watako:** Halafu sura ya kumi na mbili inahusu mazingara. Kutunza kwa misitu, shamba na vitu kama hivyo. Sura ya kumi na tatu inahusu fedha za uma.

**Com. Adagala:** Haya mazingara ya ndani yake kwa ripoti your *amagina genu yaga* pia yako ndani. Mnajua hivyo *magina yaga* ni mali. Tuliambiwa hapa ni mali *nzilianzi* wakatuambia ni *khamenya za mumagina muno. Kimenyi za mwamagina muno* na ni mali. So hiyo mali pia itazungumziwa, tutapanga tutaona vile tutapanga.

**Watako:** Sura ya kumi na tatu inahusu fedha za uma. Jinsi fedha za uma zitakavyo angaliwa na ufisadi pia imeangaliwa katika sura hii. Sura ya kumi na nne ni utumishi kwa uma, public service. Sura hii inaunda kikosi cha polisi sas itakuw polisi service, prisons pia wako hapa lakini wataitwa correctional services.

Halafu sura ya kumi na tano ambayo inaongea juu ya defense/ulinzi. Kuna sura ya kumi na sita inaongea juu ya leadership na intergrity mambo ya corruption yote yako hapo. Sura ya kumi na saba ni Constitutional commissions ama tume ambazo ziko katika katiba, tume ambazo zimeundwa ndani ya katiba.

Sura ya kumi na nane inaongea juu ya ubadilishaji wa katiba. Katiba hii jinsi itakavyo badilishwa ikiwa inahitajika. Halafu sura ya kumi na tisa ni interpretation, yaani ufafanuzi wa katiba. Halafu sura ya mwisho ni transition and consequential provisions. Hizi ni sheria ambazo ni za mabadiliko.

**Com. Adagala:** Hiyo ni muhimu sana sababu watu wako na maswali mengi sana kuhusu hiyo. Hiyo ikitoka kwa sehemu moja ukienda kwa sehemu nyingine au karne moja tuseme na unaenda kwa karne ingine kuna vitu hapo ambavyo vinafaa vilindwe. Sasa hatuwezi kusema hii imepitishwa na katiba hii impetishwa na ile imekufa. Tunataka huyu mama chamelion wanamwitaje kwa kiswahili. Huyu mama *inyambu* aishi kidogo au tuwe na njia ya kulinda huyo mtoto ili aendelee mbele. Tuwe na hiyo bridge like bridge between the two constitutions daraja hiyo ili tuvuke twende kwa station ingine. Hiyo ndiyo chapter twenty. Sasa imeeleweka, nafikiri tukifanya hivyo hata kama hautajua lingine utajua kuna sehemu ishirini na kuna vitu fulani kwa kila sehemu. Hivyo ndivyo katiba hupangwa.

Tuna vitu fulani lazima viweko katiba. Kitu cha kwanza hatukuwa nacho kwa katiba yetu ya sasa ni utangulizi hata muli-check hapa watu wakasema lazima tuwe na utangulizi sivyo. Lazima tuwe na kile kitatuongoza na iwe kwa utangulizii sivyo. Sasa na hizi sehemu zingine vitu vingine mmezungumza viko hapa. Wacha nieleze kitu kidogo vile tulijadiliana hii katiba na tukafika kwa maoni haya ambayo ni proposal. Maoni ya wakenya wote wale walifika kwa kutoa maoni iko kwa commission imwekwa kwa tape kwa maandishi na pia kwa database yaani imekwa kwa computer na wamechukuwa sasa maoni ya education ngapi wameweka katika hapo ukitaka kuona pia ya Vihiga iko au ukitaka ile ilitolewa na akina mama iko na yote ingine iko. Sasa kuna database ya hiyo yote.

Sasa kama sijaendelea database yetu wakina mama kumi na saba kutoka kwa mia asilimia kumi na saba peke nchi nzima ndiyo walitoa maoni kwa wale walitoa, 17% na hiyo ni shida kwa sababu wakina mama wako 52% na hiyo pia sikulaumu lakini nikusema ni awareness. Tukiketi hapa na wakina mama ni wachache pia kwa database watakuwa ni wachache hata kwa majina. Sasa hiyo ndiyo shida inatokea vile tutatoa ni shida za process. Lazima mujue ziko vipi si ati kwa sababu waalimu hawako hapa tuwalaumu la. Waalimu wafike ili watoe maoni yao. Ni kitu cha forward looking hii constitution ni forward looking. Sasa kile ningependa kusema ni sehemu hizi tuliangalia pia apart from the data, yale maoni tulipata kwa nyinyi tulisoma constitution za nchi zingine. Ukiwa kama una computer na email iko kwa website kama hauko nazo tulitaka ziwe kwa district co-ordinators office, lakini uwezo wetu haukutuwezesha lakini kuna kitu kidogo hapo chochote cha katiba ya nchi zingine.

**Agnes:** Kwa documentation centre yetu tuko na katiba ya South Africa, Uganda, America nadhani ya Australia mko free kuja kusema mkiwa na wakati na hiyo documentation centre iko ENTC block kwa compound ile ya D.C, not the main block but the block down. Tuko na documentation yetu hapo imeandikwa CKRC documentation centre na iko na hiyo katiba hata saa hizi. Asante.

**Com. Adagala:** Watu wengi wanajua hapo kwa District Co-ordinator office ya Agnes iko hapo iko na vitu hapo kuna katiba news ambayo ni gazeti letu linatoa news ya vile tunaendelea. Sasa kama haujafika hapo tafadhali chukua muda mfupi ufike hapo ili uimarishe masomo yako kuhusu katiba. Sasa tulisoma hiyo ukiangalia ya South Africa, India hata kwanza ile preamble nilipenda sana sio ya Amerika ili ya India mzuri nyororo fupi na ina kila kitu ndani. Yetu pia ni fupi ukiangalia preamble hapa kwangu ni page moja. Ukiangalia ni kitu kifupi sana, preamble ni kitu kifupi sana. So ni kama tuseme *amalago, indagano ijenei ni indagano kahisa* kama hiyo ya bibilia ni kumi peke sivyo lakini ina mambo yote hapo ndani halafu baadaye wanafafanua *lilago hiyo elilaog la kale na elilago liya. Hili ni lilago nilio ekipala indigano ye kipala katiba*.

Tulijadiliana tunaangalia maoni ilikuwa upande gani zaidi kuhusu elimu, na elimu watu wengi wacha niwape tu huo mfano. Elimu watu wengi walisema iwe bila malipo. Nikisema bure mtafikiri haina maana lakini bila malipo watu wengi hata hapa wengine wachache wakasema wacha wapunguze malipo iwe kidogo lakini wengi walizungumzia elimu wakisema iwe bila malipo.

Kuhusu chief watu wengi walisema chief wawe elected na wengine wakasema wawe appointed na wengine kama vile iko na wengine wakasema wakiwa appointed wapigwe transfer kama D.O’s, D.C’s na P.C’s sivyo? Sasa kulikuwa na maoni mazito hiyo ndiyo tulienukua ya katikati hiyo ingine tulikuwa tunaiweka kando hii ingine kando kidogo lakini tunaona kama inaweza kuingia. Vile unafanya sisi watafiti tunajua hivyo tunachukua majority views. Hata kwa kidemocrasia ni majority view. Na kuna mambo mengine kama provincial administration tulijadiliana sana lakini kitu cha kwanza watu walisema scrap na wengine wakasema ni nzuri sasa tulikuwa na Haji ambaye alikuwa ni P.C hapa tulipata maoni yake ilikuwa kwao Ijara, North Eastern, akasema provincial administration is very good, si unaona kwa nini yeye amesema it is very good, yes, very good and he cannot what else will take its place. Natukamuuliza natukiwa na kitu ambacho kitachukua kwa vile haiko kwa katiba, tukichukua kitu kingine kisimame kwa hivyo provincial administration itakuwa aje? Akasema la hakuna kitu kinaweza kuwa kizuri kuliko provincial adminstration na wananchi wanaketi hapo na anawasikia wanasema scrap. Hasa huko hawataki kusikia mambo ya P.C na D.C na D.O hawataki.

Haya sasa pia mnaona haikuwa kitu it was not a polite discussion. Saa zingine illikuwa kugombana sana kwa commission tulikuwa Mombasa. Hivi vyote tulikusanya halafu tukaketi Mombasa. Mimi nilikosa ndiyo unaona huyo kijana ananisaidia mengine. Nilikosa sehemu kwa sababu nilikuwa kwa mazishi ya mzee. Lakini nilienda nilitoka kwa mazishi ya mzee nikaenda nikapasuliwa jicho nikapanda nikaenda kwa sababu sikuwa naona lakini sasa naweza kuona kidogo. Sasa nikaenda nikapata wako kwa vitu fulani nikaingia hapo na hii mlifanya nini na hii na ilikuwa na moto. Sasa hakuna kitu kwa constitution lazima kile kiko hapa mimi ni-defence, lazima wewe uwe umejadiliana to the point of defending kile kimesikika. Katiba iko hivyo si kitu vile kila mtu anataka ni mwishowe ni consensus.

Nafikiri Maragoli *mwamanya papola gugila ndi msaguru nikufuminyana*

**Audience:** *Kufuminyana*

**Com. Adagala:** *Kwadiga apundu kuduka kosi kudiki kupola okay. Kada ijapudiza kufumi.* Si hiyo ni mila yetu. Haya

tukafika hapo na sasa ikawa kuandika, tukaandika pia lakini kila jambo tulizungumzia tukajadiliana tukagombana, hasira wengine wanatoka lakini watu lakini wale hawakuweko kulikuwa na commissioners wengine hawakuweko sijui watasema nini. Kwa sababu hawajui tulifika kwa haya mambo vipi. Hao ndio walikuwa ni majudges. Turn off your mobiles please. Walikuwa na judges wanapeleka commission kwa court. Sasa hatujui watakuwa wanasema nini kwa sababu wamerudi kwao kwa watu wao *ewapo no palomelome mupao* sasa hatujui watasema nini kwa sababu imeandikwa. Na ndiyo tunasema kitu ikiwa kinaendelea usikae kando kwa sababu mwishowe kitatokea halafu utafanya nini.

Nataka sasa kusema sisi constitution ni draft bill. Simunajua bill na Act haijakuwa Act. Haijapitishwa kwa bunge bado ni majadiliano na mtu amesema pale tungekuwa na muda mrefu wa kujadiliana tungeweka hiyo proposal sasa hiyo ndiyo tunaendelea. Ni majadiliano hata hapa tunajadiliana lakini mjue tulichukua ile juu ya majority tukiendelea. Watu wa N. Eastern walituambia hawa refugees tumechoka nao, Waturkana wakasema hao watoto wao wanasema shule nzuri, elimu nzuri hata kuliko yetu tumechoka lakini kwa international format ile katiba inaundwa natuli-sign hiyo mambo ya wakimbizi tukaweka hapa refugees na vile wamefaa wakae. Kwa sababu refugee anavuka mpaka, sivyo sasa ni international sasa iko hapo pia. Wacha nieleze tu hivyo sasa watu wa N. Eastern sisi hatujui hiyo mambo wanasema hawa watu wanakata hii miti, kuni, wanaishi wengi hapa na kule watu hawaishi wengi kwa sehemu. *Pandu pamanya apengi da apandu za apandu adi khandi ni apandu penza papugula dadabu hiyo na …(inaudible)…*. It is a big section na Turkana ina big sections wanaisha sasa ni watu wengi sasa. Sasa wanaharibu mazingira, wameharibu mila. Sasa inafaa waishi vizuri na wengine sasa hao watazungumzia hiyo zaidi na sisi tuzungumzie yetu na huku tuone inaingia vizuri lakini tukumbuke tuko kwa taifa.

Kulikuwa na swali hapo lakini nataka tuanzie preamble utangulizi, tuingie ndani sasa. Swali ilikuwa hapo ilikuwa ya?

**Jorama Amali:** Commissioners na wananchi hamjambo. Nadhani ni kitu kizuri commissioners kikuja mara ya mwisho kusikiza maoni yetu. Kuna sehemu moja tu ambayo ningetaka tujulishwe. Wakati mliandika hiyo recommendation ni kitu ambacho kweli watu wengi walikuwa wanataka na …(inaudible)…. Nilipokuwa nikisoma article hizo, article two and nine.

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Amali:** It is alright I just… mwisho kabisa.

**Com. Adagala:** …(inaudible)…okay lifungue hapo ndani, preamble. Wacha nione kama …(inaudible)… tumesema tuko kabila nyingi tunajua hivyo tunakubali kuna diversity ya kabila nyingi kwa sababu kwa ile ingine hawakusema kuna kabila nyingi. Tunajua kuna Waturkana, Wadigo, Wamaragoli, Bukusu na Pokot kwanza hao ni watu moto moto sana tunajua hivyo kwa preamble tunasema tunajua, tunaelewa tunakubali. Tunajua kuko na familia jamii na taifa, tunashangilia tuko committed. Tunajua kuna familia sasa familia ikisemekana hivyo kwa katiba imekuwa entrenched community iko entrenched na nini ingine, na pia tumechukua hiyo sub ordinance wale tunasoma kwa kingereza naeleza wale wengine pengine hawasikii demokrasia, uhuru, rule of law ina hiyo social justice hiyo yote pia tumeweka ukiwekwa hivyo kwa katiba lazima idumu sio kitu tunasema halafu itaenda mahali ingine halafu itakuwa tofauti hivyo itadumu.

Kuna ile haki ya wananchi imeanza na "we the people of Kenya" naona hiyo katiba ya leo haisemi hiyo. We the people nguvu za katiba, nguvu za Kenya zimetoka kwa wananchi. Sisi wananchi wa Kenya sasa hiyo yote inasema sisi wananchi wa Kenya hapo exercising ile haki yetu na haki ambayo huwezi sasa kuleta maswali juu yake ni ile ya tovu. *Papola opeku kugindu gii mulurela hhii ni haki ya muliwela kwa sababu umezaliwa Mkenya na uluvola lulivo lapikwa Mkenya zikape* ndio hii ni haki, haki yetu ni hiyo hakuna mtu anaweza kukwambia huwezi kua na tovu au hauna tovu kwa sababu haungezaliwa kama hauna. Hiyo ni alienable.

Sasa tunatengeneza, tumetengeneza na tunatekeleza hii katiba kwa sisi wenyewe na pia kwa vizazi vijavyo. Katiba sio yetu peke yetu. Ndiyo mlisema wazee sisi watu ambao tuko over fifty you have to think it is not for now peke yake ni vizazi na vizazi na vizazi hata wakitengeneza ingine watajenga kwa msingi huu vikienda mbele. Hata sisi wenyewe vitu vingi tumejenga na ile katiba iko. Halafu Mungu uibariki Kenya kwa kiswahili mnasema hiyo na kwa kingereza na kwa sababubu wananchi walituambia lazima Mungu awe kwa katiba yetu. Mlisema au hamukusema? Mtafika mahali mgeuke tulichukua maoni Munge awe kwa katiba yetu na tumesema God bless Kenya. Tulikuwa na drafts nyingi za hii kwa sababu mimi nilikuwa kwa kamati ya constitutional process. Ingine ilianza na hiyo ya kwanza eh Mungu yetu. Oh God of all creation tukasema no wacha tuweke ile hapa chini ndio wengine wakiwa supremacy of God tukaangalia halafu tukaweka hapa God Bless Kena. Watu wengi walituambia Kenya ina shida kwa sababu Mungu hayuko kwa katiba yetu ndiyo hapo tumeweka. Point yeyote kuhusu hiyo preamble imeeleweka.

This is our guiding light, this is our vision, this is how Kenya will be it has talked about the unity that you told us it has talked abou the sovereignty of the people. Preamble, any question? Halafu tunaenda hapa sasa ni ukuu wananchi na wa katiba. Ninawambia kuna vitu viwili watu na katiba. Katiba inatoka kwa watu, katiba inalinda watu hivi vitu vingine vinapata nguvu kutoka hapo lakini vile katiba yetu ile ingine ilikuwa kama inatoka kwa serikali ndiyo inakuja saa ingine haikuleleweka inatoka wapi. Lakini sasa ni vitu viwili hapo, nguvu kuu ni nguvu za watu, za wananchi bunge, mahakama na urais wote unapata nguvu kutoka kwa wananchi. Hiyo sovereignty ya bunge, ya urais na ya mahakama inatokana na hiyo nguvu. Ndiyo hiyo inasema hiyo nguvu ya katiba.

Constitution huwezi kuichukua tu na kufanya vile unataka nayo, lakini unachukua hili …(inaudible)…good governance, utawala wema, haki za binadamu, rule of law, ukuu wa sheria, kitu chochote ambacho hakiingii hakiambatanai na katiba, katiba iko juu yake, hiyo ndiyo supremacy hiyo wakalia juu yajivyo vitu vyote vingine. Mahakama lazima itekeleze katiba na pia tutakuwa na commission courts zitafanya hivyo commission tutawaeleza baadaye. Natukiendelea, hiyo kupinga katiba kutakuwa na bunge italeta sheria ambayo itaambatana na katiba. Vitu muhimu ambavyo vinakuwa kwa sheria ya Kenya, cha kwanza ni katiba.

Kuna mtu ambaye anafaidika na hiki kiswahili au tuendelee kwa kingereza. Nataka kujua tuendelee kwa kingereza au la. Nataka watu wenyewe waseme yule anafaidika ni nani. Weka mkono juu ili nijue kwa sababu tunaweza. Kitu cha kwanza kwa sheria za Kenya ni katiba halafu hiyo sheria ya bunge, halafu sheria ya kiafrika ya utamaduni zile ambazo tunazo kwa jamii yetu hiyo ya Kiislamu na pia hizo zingine za Kihindu halafu East African community, wale sasa tuko Kenya, Uganda, Tanzania pia

sheria yake inaingia hapo. Na pia, hizo zingine wamerudia customary law. Customary international, customary ile ya kimataifa hizo treaties na vitu kama hivyo. Sasa hiyo ndiyo sheria ya Kenya sas inaanza na katiba inamalizika na ile ya international. Now, kuna swali hapo …(inaudible)… njoo.

**Fanuel Kaiga:** Nilikuwa nimesema jina langu. Niseme tena?

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Kaiga:** Fanuel Kaiga. Langu limetokea tu kwa mazungumzo na hasa mahakama, court. nataka utueleze kidogo vile mmepitisha namna gani kwa sababu kwa wakati huu mimi sioni korti zina kazi kwa sababu watu wamebuni korti zao na sijui mumesema nini kwa maneno hayo. Yaani mkienda kwa utawala wametengeneza korti zao mpaka ulipe pesa kwanza ndiyo wasikize kwa maneno yako hapo mmesemaje?

**Com. Adagala:** sasa tunaguzia juu chapter. Una katiba kweli? Sioni kama una katiba. Tulipokuwa tunapitia ulikuwa unaaangalia, tafadhali tuende utaratibu hiyo ni chapter nine okay kama ile ya mzee Amadi itakuwa na nafasi yake lakini tumeelewa. Patricia sijui unataka watu wanauliza maswali wafanye aje.

**Patricia:** …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Committee can you assist in that, committee, mmoja, chairman tupe committee member mmoja ambaye, kuna mtu mbali kule.

**Bulira:** Mimi ni Abedi Bulira. Hiyo chapter ya kwanza hiyo number two. The last bit of the first chapter mimi naonelea mmeweka hapa parliament baada ya miaka miwili after this constitution would have been put in effect or enforced, parliament itakaa na tena ibadilishe. Mimi naonelea muda wa miaka miwili ni muda mchache zaidi. Ni jambo kama hili ndilo lilitufanya tukaharibu hii constitution ambayo tunataka tuiwache. Revising it, every now and then mimi ningefikiria pengine baada ya miaka hata ingawa wakati mwingine nilisema miaka ishirini lakini wakati huu wacha iwe baada ya miaka kumi ndiyo turudie kwa constitution yetu tuone ni jambo gani tunaweza kubadilisha.

**Com. Adagala:** Thank you very much. Hiyo hapo, kuna ile bridge, ile daraja ya kuvuka kutoka kwa constitution ya sasa kuenda kwa ile ambayo iko proposed na kuna hiyo vitu iko na constitution mzee. There is something called transitional and consequential. We are in a transition there will be things which will need to be done in the transititon. Halafu hiyo vitu vitakuwa na consequences. If we say for instance provincial administration is not there although it was never there what happens. What will happen to this D.C. building? You see it is more serious than just things of the mind. What will happen to the D.C’s building? What happen to the P.C, chairs in their offices? Na here what they are saying because we know that there will be a need to harmonise laws between the old and the new that transition siyo hiyo ya kubwa ya revise tena naelewa unasema ile kubwa yenyewe.

Ile bridge hiyo ndiyo ya two years na iko kwa schedule siz ukiangalia nyuma ni nyuma kabisa schedule six nafikiri wewe ni musomi utasoma uelewe. Kuna vitu vingi ambavyo vinasemekana kwa schedule six. Parliament will need to harmonise laws they will need to look again what we are doing now is okay but they wll be those little things they wil have to go through with a tooth comb, toothpick, polish and make sure they rhyme and harmonise. Hiyo ndiyo, two years isn't that so.That is the one that is being talked about.

Lakini lile umesema kitu kiliharibu katiba yetu ni hiyo kufungua kufungua na bolt hapa unaweka musumari ingine hapa unavunja ukuta huku huyu kufanya hivyo ilifanya katiba ya Zimbabwe wakaweka, it shall not be ammended for 10 years kwa sababu vile sisi tulifanya, tulifanya chokora mbaya sana. tuliharibu vibaya sana hata ni aibu hii katiba watu wanaangalia kutoka nchi zingine wanasema hii ni nini. Sasa hiyo ndiyo wewe unasema na sijui kama kuna mahali hapo lakini weka hiyo chini. Nani anaandika hizo recommendations ili tujue people said it should be once in a generation. A generation is 25 years some people said 50 years, some people said 100years, some people said 10 years like you. Tthat is a proposal this is why we have this meeting here kuelewa na pia kutoa maoni zaidi na asante sana pia wale wengine wametoa na ile ingine ambaye inakuja pia tutaenda chapter by chapter itolewe.

Will you read schedule six and see how those laws we will go through them if we do it now it will mix us a little bit but I wanted you to know that laws will have to be harmonised haya asante umetosheka lakini hiyo proposal yako ingine usiipoteze. Haya tuendeleee. Hii ndiyo Jamuhuri ya Kenya chapter two. Kwanza hii katiba ya sasa ilisema Kenya is a sovereign republic halafu ikawacha lakini tumechukua hiyo kwa sababu lazima iwepo kwa katiba hiyo sasa imekuwa chapter nzima na hiyo jamhuri ya Kenya inatoka wapi inaundwa vipi? We said we the people who are within the republic lakini ile ingine ilianza tu na republic sasa ileiko tu kwa katiba ya sasa ni ramali ya Kenya haina watu ndani ni kweli ni kitu kizuri. Ndiyo unaona tukizungushwa vile tunazungushwa kwa haiko kwa katiba ya sasa.

Wananchi hawako kwa katiba ya sasa. Sasa itakuwa multi-party hiyo tulipigania hiyo, yaendelea itakuwa ile ya kushiriki shirikisho kitu muhimu sana, wananchi watashiriki, hakuna mtu atawachwa nje lazima ushiriki na ujue itakuwa vipi. Hiyo tumepigania neno nzuri sana kwa kiswahili transparency. Kuna neno nzuri, iko kwa katiba wameweka translation ya kiswahili na accountability na tuatakuwa na hiyo ili mtu asingilie kazi ya mwingine kule juu ya bunge, mahakama na urais wasingiliane sasa wanaingilia sana na wengine wamechukua nguvu za wengine na wengine wamejiona wao hawako chini ya katiba kila hiyo sehemu iko chini ya katiba na hiyo moja na haki ya binadamu na pia sheria kutawala.

Territory yetu imekuwa hapo unaweza kuangalia wale wako mpakani hasa ndiyo wanahusika na hiyo ni first schedule kama unapata hiyo ni first schedule. Hiyo ndiyo the first schedule ya republic. Republic ni nini? Okay hiyo mambo ya schedule ni ya kisheria ita-describe boundaries of Kenya and what in Kenya. We shall look at it afterwads.

In the present constitution hakuna kitu capital ya Kenya iko wapi, Nairobi inaishi tu kwa sababu tunaenda Nairobi lakini inafaa iseme capital iko wapi na iseme hapa ni Nairobi. munakubali? Capital kulikuwa na wakati mwingine walisema Nairobi iko mbali huko iende Isiolo au iende Nakuru na Tanzania walibadilisha yao ikaenda Tanzania ikaenda Dodoma hawakujenga sana

kwa sababu ya ukosefu wa pesa. Nigeria walibadilisha ikatoka Lagos ikaenda Abidjan na wamejenga kwa sababu wako na pesa za petrol walijenga. Language za Kenya, hiyo ni capital inafaa ijulikana lakini kitu muhumi hapa inasema in line to decentralization the headquarters of national government departmentrs and national public institution shall be decentralize to all the provinces equitably hiki kitu equitably kwa constitution ni muhimu sana.

Inasemekana sio headquarters zote za vitu vyote viwe Nairobi, South Africa wamefanya mahakama iko Johannesburg, bunge liko Pretoria, serikali iko wapi sasa ndio watu wote wanashiriki lakini hii iko hapa sasa na pengine kuna ministry huenda ministry moja hata watu wa western walisema ministry ya agriculture inafaa iwe headquarter western part of Kenya, North Rift kwa sababu hao nidyo wakulima zaidi munaona kitu kama hicho. Na wengine wakasema tourism iwe Mombasa mnaona na inafaa iwe tourism iwe kwao kwa sababu wao wanasema wao ndiyo jimbo la Kenya wakisema Maasai wanajua ni Kenya. That is a very important point it goes with devolution. Mzee wa devolution inaenda na hiyo. Official languages, Kiswahili na it is important that Kiswahili is one. Kiswahili and English, then the national language Kiswahili it means from now on everything will have to be in English and Kiswahili. Hansard kwa bunge hata ukizungumza kwa kiswahili wanatranslate wanaweka kwa kingereza lakini sasa lazima iwe na hansard ya kingereza na kiswahili record ya bunge. Notices hata hizi vitu mnaona makaratasi ya serikali lazima itakuwa kwa lugha mbili.

Tulikuwa na jambo hapo na pengine mungefikiria vile kwa devolution kuna district tutaeleza hiyo na watu wengine walikuwa wanasema wanataka lugha zao zizungumziwe kwa district representative house, kwa sababu tutakuwa na representative wa district lakini tulizungumza mimi nilikuwa mmoja wao nilitaka Kiluyha kiwe Vihiga na Kimaasai kiwe Umasai kwa district lakini tulishindwa na tukakubaliana hivi ndivyo litakuwa Kiswahili na Kingereza …(inaudible)….. Lakini nasema hapa serikali italinda lugha zetu zote kwa sababu ni nyingi tuna-recognise hiyo diversity.

Hakuna dini itakuweko dini na serikali zitakuwa tofauti na jamuhuri itakuwa tofauti hayo ndiyo iko kwa nchi zingine nyingi lakini ukienda kama Iraq inakuwa Islamic Republic si mmeona hivyo. Ukienda mahali pengine unapata iko such and such na zingine pia lakini sasa tunasema sisi tuna diversity na hakuna ile itakuwa chini itakuwa ya serikali hiyo ndiyo point ya pili hapo na ya mwisho. Dini zote zitakingwa kwa usawa. Hakuna moja itakuwa kubwa hakuna moja itakuwa sasa Friends church ndiyo dini ya serikali, hakuna kitu kama hicho kama Vatican. Vatican is a Roman Catholic state hiyo iko hivyo lakini kwa hii tunasema hiyo yote itakuwa separate.

Kuna hiyo national symbol nafikiri mnaweza kusoma. Bendera, wimbo wa taifa hiyo kirauni na kuna hiyo muhuri wa taifa hiyo ndiyo symbol kielelezo au nini, ishara ya nchi. Kuna oath za Waquarker wale mmeketi hapa mnajua sisi hatuapi kwa bibilia hiyo hiyo inaitwa affirmation. Sasa hiyo affirmation pia iko wale hwataki kuapa kwa bibilia au kwa koran upo. Hiyo itakuwa kwa fourth schedule wanaweza kuangalia 4th schedule. Wacha tumalize ndiyo …(inaudible)…. Yes atauliza tukimaliza. Haya kuna holiday tulizungumzia sana. National holidays zitakuwa madaraka day, June one, Jamhuri day 12th December and the date ile siku katiba itatengenezwa itakuwa pia national day, itakuwa katiba day, hatujui itakuwa siku gani. Si mumeleelewa. Okay swali, mheshimiwa ungependa pengine ungeweza kusimama kwa wakati huu wacha mzee aulize swali halafu…

**Arthur Adenga:** Asante sana commissioners na commission members na wengine. Jina ni Arthur Adenga ningependa kusema kitu juu ya hizo topics tumepitia. Sijui kama tunaweza kuweka kitu kuhusiana na appearance on the currency, the national currency. Ningependelea hizi pesa ziziwekwe muhuri wa kiongozi kwa sababu tuatendelea kugeuza viongozi kila wakati.

**Com. Adagala:** maoni ilikuweko kweli kuhusu hiyo. Sasa pia tumeandika hiyo. I hope you are writing them. Tutaweka hiyo, lakini nieleze bila kupinga upande moja au mwingine kama U.S.A ambayo umekuwako muda mrefu wana viongozi tofauti tofauti kwa shilingi kwa ndururu, kwa dola ya dola hiyo ni kiongozi mmoja, dola kumi kiongozi mwingine lakini hao wamekuwa na viongozi wengi. Shida yetu, tumekuwa tu na viongozi. Haya nafikiri unatoka ten unaenda fifty dollars another na pia wanasema kichwa chako hakiwezi kuwa kwa pesa lazima iwe imepita miaka hamsini. Sasa kama Kennedy, hayuko isipokuwa walimpenda lakini nasema lazima miaka hamsini ipite ndiyo uweko lakini hiyo tutarudi kwa sababu watu wengi sana walisema nini. Asante sana kwa kutujulisha hiyo mheshimiwa.

**Hon. Yusuf K. Chanzu:** Commissioners na co-ordinators na wale wamefika leo hamjambo? Mimi sitakuwa na mengi ya kusema, nafikiri tutakuwa na nafasi wakati nikimaliza hii kazi kuweka maoni yetu wakati hii ikija parliament. Lakini kwa wakati huu, ya national consitututional conference sasa ile labda mawili ama matatu tu nikuwakaribisha maana mko Vihiga constituency ni kuwakaribisha commissioners na wale ambao wamefika siku ya leo kusikia yale ambayo walisema na kuona kama ikiwekwa kwa hii draft na kama haikuwekwa tena tuko na nafasi ya kurekebisha kidogo kidogo. Na kitu cha pili ni maoni kidogo kidogo tu nafikiri we can take it into account maana tumekuwa na open forums, huu ndio wakati wa kwanza although ni the 2nd time kutengeneza constitution ya Kenya kila mahali kupeana maoni yao. I think *nigashadabehe* I commend your commission for this because kila kitu lazima iwe na mahali ya kuanzia huwezi kusema itaanza halafu yote iwe sawa.

That, for us sisi ambao tuko kwa serikali ambao tunajali yale masilahi ya wanakenya mimi nafikiri hii ilikuwa njia nzuri ile ambayo tumesikia kidogo kidogo, ati hii constitution draft labda mmesikia imekosa na maneno mingi ati ilikuwa imeandikwa mbeleni halafu ikapeanwa hiyo ilitokea huko Nairobi. We have not gone there hatujaingilia sana kuona kama ni kweli lakini bado tuko na tume ya kufanya hiyo correction. Juu walisema waletee hii hapa mashinani tena watusomee ili tuende through one by one tuone kama iko mahali tunaweza kurekebisha and for me Mr. Commissioner vile ningependa tu kusema umejua saa ingine watu wakipeana maoni mmepeana maoni tunajadiliana hivi lakini ikiandikwa saa ingine inatoka tofauti kidogo that is what we need to correct.

Duniani kila mahali tumekuwa na reforms mabadiliko lakini hiyo mabadiliko saa zingine ikiwa exercised tena inaleta shida. Hata hapa Kenya wakati huu tunaona from 1997, au tuseme vile president alisema from 1992 wakati wa kuleta vyama vingi halafu, 1997 tukiwa na IPPG parliament ile ilikuwa inasema tuondoa nguvu za assistant chief. Chief's Act hatuwezi kuona sana lakini sisi kama viongozi tunaona dalili ya shida kwa maana population kama ya Kenya tuko na vijana wachanga between age of 20-30. Si hata, ukipita mahali watu ambao unakuta wakati huo wanasimama barabarani ni kijana kama wa miaka hiyo. You have nothing to confront them and majority ya population 77% it is going to be a problem ndiyo wakati ule tukiongea nilisema, we must look at lazima tuangalia sheria ambayo inaweza ku-take care of that situation. Kwa maana wakati huu kila kitu ikitokea

na kisiasa mnajua ile ambayo inafurahisha watu sana ni ile ambayo inazuru serikali yaani inazuru authority. Kama wakati huu mtu akianza matusi kwa huyu kwa commissioner amekaa hapo bila ya control utakuta kila mtu ametoka kwa village kuja kuona, lakini wakati huu they cannot come because they know you are dealing with a tough thing you are thinking. Mnatumia fikira that is why you cannot see small children here. Lakini ukianza hapa matusi na kutukana huko nje utaona wengi wamekuja kujaa hapa kuja kuona.

Therefore, I was saying that these reforms are giving us trouble particularly those who are in leadership even we are seeing lack of respect from people, lack of respect for the leaders so, I just want us to look at these reforms again particulalry this thing of provincial administration. I think what we were talking about vile tulikuwa tunasema nafikiri kupat kitu ambayo inaenda kuwa all inclusive. Such that at the same time tuko na administration hapa na tuko na ile ambayo inaweza kujenga area kama ward iwe pamoja and then.

Ile ingine tena nimeona mtajadiliana zaidi am just saying a little but …(inaudible)… I have not concentrated mine lakini ni views kidogo. Ile ingine ni hii ya MPs. Vile tunasema tuwe 210 MPs ambao watachaguliwa for constituency na tuwe na wengine 90 ambao watachaguliwa na parties. 90 is a very big number, na ukichukua 90 ikichaguliwa na parties hii inatoa ile ambao hii constitution inajaribu kufanya wakati huu. Tunajaribu kupatia wananchi demokrasia kubwa ya kuchaguwa, so if you take 90 which is also 1/3 inachaguliwa because in total it will be 210 which will be 300 that is almost 1/3. So hiyo tena may be, in the long run, maana mnasema tuwe na time ya kukaa kabla ya kufanya ammendment . So we must look at that in terms of long term, maana inaweza kuleta shida tena. I think the number is too high. Na tena ile ambayo nimeona tena ambayo tena expect the cost. The cost of this is going to be we have been talking about kila wakati tumekuwa tunajadiliana kila wakati tunasema tuko na umaskini tunataka katiba ambayo inaweza kutupunguzia gharama. Ile miradi au ile miendendo ambayo inaweza kupunguza gharama kwa wananchi kwa maana ikiwa mingi gharama tena ni kwa wananchi kulipa itatoka kwa tax payers money. So, ni wananchi watagharamia hiyo so it is going to be costly. And then the other aspect

**Interjection:** Wawe wangapi? Give us a number.

**Hon. Chanzu:** Actually I didn’t see anything wrong with what we are having at the moment in terms of numbers.

**Interjection:** …(inaudible)….

**Hon. Chanzu:** You know what we have done in the past with the 12 it was almost the same because the parties which had the majority more numbers in parliament they were the ones which were nominating on proportional basis that is what they were doing but it is for you to decide but am only saying in terms of costs and increasing the amount of leadership at the top when we want to cut down. Lakini mtajadiliana, mtaona because sio sisi peke yake tunajadiliana hapa tuko na wengi constituency zingine pia wanajadiliana. Lakini maoni yenu inatufaa. And then I have talked about the provincial administration hii devolution of powers, vile nimesema that is what I was saying it was intended that it is going to be costly. Wakati mtafika kwa hii sehemu ya villages, village councils na vitu vingine mnasema tunataka ku-reduce costs sasa tukiwa na councils it is going to be so

bureaucratic. Itakuwa na village lakini we must have a level which will follow optimum or something ile ambayo inaweza kufanya control na maoni ya party inakuwa kwa the elders we have under the chiefs and so on.

These powers ya president, kutokana na yale mlisema mbeleni in a developing country kama Kenya na population ambayo inaenda juu na tuko na communities nyingi mimi naona inakuwa ngumu kuwa na president ambaye hana power ya kutosha. Kwa maana inaweza kuwa chanzo ya shida everytime kwa maana ana vipawa kwa agency all the time …(inaudible)… but I don’t know we will discuss it again but that is my view. Can I ask it clearly let us look at whether am not ready to do everything even kwa hizi councils ambazo we are devolving poers zile ambazo zinaweza kutusaidia to create employment and to reduce poverty. So that is the intention of bringing powers from up there. But at the same time lazima watu wawe na njia ya kujipatia mali na vile ya kukaa.

Recalling of MPs not because am an MP but the method we have come up with in the document here tena naona kama inaweza kuleta shida. I think since we are maturing, tuna-mature na democracy lazima watu wapatiwe enough time kama ukichagua kiongozi kama vile tulichagua commissioner Adagala Kavetsa, lazima you must put in a lot of effort tuweke ndani time a lot of thought. Mkichagua mtu asiwe mtu ambaye mnaweza kusema tu kesho yeye because of learned team and many things in our place you can find many people grouping up in a majority in one area na ukute they are moving something which can go through because of members. Because Kenya has a problem of …(inaudible)…. Unaweza kukuta only one clan is saying that now we are removing so and so because they are large in numbers because only talking of 31% . So mimi nafikiria you have to think again tufanye criteria tukichagua mtu, tumchague but of course the penalty is normally very high when somebody is removed from a job of responsibility, he feels the pain even if it is 20 years even if it is 30 years, he feels the pinch so hiyo ndiyo nilikuwa nasema tunaweza kuangalia tena tuone kama tunaweza kurekebisha.

I think ni hayo tu for now, sitaki kusema mengi kwa maana nimesema nitakuwa na nafasi ya kwenda …(inaudible)…. But ni vizuri kuja kuhudhuria mkutano kama huu, kwa maana katiba is everything for us every country katiba ndiyo msingi ndiyo, frame ambayo kila kitu ambaye inaendelea kama mkisikia tuko na lawlessness katiba si nzuri kama mnasikia wafanyikazi hawafanyi vizuri it means the laws somewhere are not …(inaudible)…. So it is the foundation of any nchi yoyote duniani so ni kitu muhimu tuwe hapo.

Then, we were saying like this, mbeleni tulikuwa tunasema constitutional review isiwe pegged, isiwekwe pamoja na hii parliament wakati huu kwa maana hii constitution vile mtu amesema ni constitution ambayo inaenda sasa miaka mia mbili, miaka mia tatu it is not for the 8th parliament. Na vile saa ingine watu wanapeana maoni ni kama hii constitution ilitengenezwa targeting 8th parliament, it should not be like that. Nafikiri hiyo ndiyo inafanya wenzetu wakisema na mimi naunga mkono kama tume is not there na tuingilie hii tuangalie from chapter to chapter, section to section. Tunataka tuwe na enough time kama haiwezekani kumaliza on time there is no point of rushing something which is going, itakaa miaka mia mbili kama American constitution. So we are saying kama haiwezekani kura iendelee mwaka huu vile ilikuwa imetarajiwa na constitution kazi yake iendelee commission kazi yake iendelee. Hiyo ndiyo nitapendekeza parliament when we go back to this subject. Kama ikiwezekana fine

lakini kama haiwezekani the commission should go in reviewing to us kwa maana tutakuwa na majadiliano mengi wengine wanasema commissioners wanataka wakae kwa kazi kwa maana wako na mshahara kubwa na maoni mengine mtu anasema hataki constitution anataka constitution isiendelee sana kwa maana hawataki president aendelee. So you see a lot of things left and right lakini hata commissioners wakipata mshahara wakati huu kwa hii contract period lakini constitution ni kitu ambayo itadumu miaka mia mbili. I think it is much better. So I think Mrs. Adagala that is what I have to say and wish you the best of luck. I wanted to rush so that I can be in parliament in the afternoon.

**Com. Adagala:** Asante lakini mheshimiwa ngoja kidogo. Unajua sijui itakuwaje sababu sehemu zingine tunaenda na mbunge anakaa na sisi hata tulipokuwa tunafanya hearings au civic anakaa siku mbili tatu hasa unajua tunakuwa na gap between kile watu wanasema kwa sababu uko na right yako pia uko leader. Sasa unajua una kazi zingine na vitu muhimu lakini wacha tuwache tu hivyo tutakuwa na nafasi ingine today then we go to Sabatia you catch your time. Walikata muda hawa …

**Interjection:** …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Actually, it was supposed to be three hours but I see that it cannot be three hours but if it just got a gap between the leader and the people. Sasa wacha nikupe Vihiga constituency report ambayo tulipata tulikuwa na watu wengi hapa *kidundu shelatswi* walikuwa wachache sana lakini ni ripoti namba 166. So this is to you. Hii ndiyo commission bunge commission district co-ordinator committee. Wewe fanya vile unaweza.

**Interjection:** …(inaudible)… (clapping)

**Com. Adagala:** Tuna mambo yote hapo hata mambo ya mawe na msitu pia iko asante. Swali lingine kwa hiyo schedule? Kwanza turudi nyuma schedule three it is addendum schedule ni kama addendum, addition kwa sababu vitu zote viwezi kuwa hapa na tena kuna sheria nyingi haiwezi kuwa hapa hii ni mama ya sheria. Hii ndiyo kuku yenyewe, halafu watoto watatoka kwa sheria za Kenya. Page 17, the third schedule is to do with the national symbols. Hiyo national symbols ukitaka kujua juu zaidi ya hiyo national symbols utasoma hapo na mzee ambaye amezungumza kuhusu pesa currency pia tutapeleka hiyo pia tuone ilikuwaje na pia itazungumziwa NCC. Maswali hapo fupi fupi usiende kwa maelezo sana. chukua wale ambao hawajazungumza.

**Interjection:** …(inaudible)…

**Ndolo Asasa:** Asante sana mimi ni Ndolo Asasa. Mimi niko na maoni mawili tu. Kwanza, ni kuhusu national oath an affirmations kwa oth schedule, oath ya vice president inaisha kwa kusema kwamba atazingatia his secrecy, neno la mwisho pale ni secrecy. Mimi ningependelea hii maneno secrecy libadilishwe ikuwe na confidential maana inafika mahali pengine tukataka makamu wa rais apatiane maelezo kuhusu rais na ikiwa ni secrecy hatapatiana. La pili ni national day ningependa kwamba national days kati ya zile siku tatu ikiwa itawezekana pia tuongeze heroes day siku ya wale walipigania uhuru wetu na wale wengine pia ni heroes hata wakati huu ambao wanapigania uhuru mwingine.

**Com. Adagala:** Wewe na mimi tunasikilizana lakini nilishindwa kwa majadiliano lakini watu wengi walisema it should be

freedom fighters day or heroes day sasa tutasema bado watu wanasema hivyo …(inaudible)… wale ambao hawajazungumza.

**Onzere Oberi:** Mimi ni Onzere Oberi nauliza upande wa dini. Dini zinakuhabiwa ukweli katika Kenya lakini uchunguzi wa kwanza kabla ya kusajiliwa ama ni hivyo hivyo tu. La pili dini linaweza kupewa nafasi ya kufanya mambo yao katika kanisa ama wazurure barabarani na makelele kama vile wanafanya na kuharibia watu wengine mambo yao. Asante.

**Com. Adagala:** Ulisema hivyo, sasa huwezi kusema kuzurura kwa sababu kila watu wana njia yao ya kuabudu. Huyu ni Mungu sio P.C. Huyu ni Mungu na njia mingi za kumuabudu tukianza hivyo mwishowe watu wengine walikuwa wanasema kuwe na dini moja tu na wewe unajua hatutaki wakisema kwa Quarkers wasiwe na silent meeting itakuwa aje? Au wakiambiwa wapende wasiwe wanapiga ngoma itakuwaje na heshima kwa dini zingine lakini tutaweka hapo unasema wawe wanaoabudu wapi hiyo pia unajua ni kanisa ni temple, msikiti. Sasa tutaweka kama maoni lakini pia heshimu ile tuko nayo hapa ni maoni ambayo watu walichanga ukiongeza au haukuweko peana ile heshima kwa ile iko lakini tumeandika mzee …(inaudible)…

**Caleb Juma:** Asante sana commissioner upande wa makanisa.

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Juma:** I just want to put maoni yangu ni kwamba, niendele tu. Kwa hivyo commissioner I just want to say upande wa makanisa. Jina langu ni Caleb Juma. I want to just make a comment upande wa judges and the constitution. My proposal ingekuwa kwamba limekuwa na limit ya makanisa because actually there is freedom ya makanisa lakini ukiyapata makanisa moja tu open na sehemu zingine makanisa hayawezi hata kujengwa hata na serikali kama unawezekana kuliko kuachia watu binafsi sababu watu wana-abuse kwa sababu every person anataka kuanza kanisa yake.

**Com. Adagala:** Hiyo ndiyo tunasema ku-streamline harmonise tunasema hakuna kanisa au dini ya serikali sasa pia haitakuwa na kanisa ndiyo hauwezi kusema hapa hakuna dini ya serikali halafu useme huku ingine ijengwe na kanisa. Na pia kuna kitu kingine kinaitwa freedom of expression, kitu hicho ndio kabisa katiba freedom of expression na ndani ya hiyo iko freedom of worship/religion. Hiyo tuliangalia tukasema …(inaudible)… freedom of religion or worship pia tutakuwa tumelimit freedom of expression na katiba yetu itakuwa kama imetengenezwa na wajinga ikiwa na limitation of freedom of expression lakini tutaeza hiyo imekuja tena …(inaudible)… okay?

**Kegode:** Mimi langu, mimi kwa majina naitwa Nahashon Kegode. Mimi nauliza hivi, mzee yatima …(inaudible)… Ningependa watu watatu katika …(inaudible)… wilaya …(inaudible)… hamjafika pahali lakini hayamo.

**Com. Adagala:** …(inaudible)… msipoteze haya, wa msiwho …(inaudible)…

**Jeremiah Macheso:** Jina langu ni Jeremiah Macheso nauliza hivi. Kuna mwaka ingine ilikuwa Section 2A iondolewe

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Avedi Bulima:** Mimi ningali hapa kwa dini wegine wamezungumzia jina ni Avedi Bulima sehemu ya tatu 'the state shall treat all the religions equally' kitu ambacho nauliza ni kwamba baru ambayo ilikuwa kwa dini ya musambwa imeinuliwa, has it been lifted? Two, wakati mwingine nilizungumzia hapa mambo ya devil worship? Devil worship pia inapewa freedom ya kufanya mambo yao. Constitution hii itakuwa ikitumbuiza kutuweka kwa shida.

**Com. Adagala:** Asante unajua hapo mbeleni tumesema African customary isn't it? Sikilizeni ili mazungumzo yenu iendelee sawasawa. Tumesema African customary na pia hiyo swali ilikuwa sasa hiyo inaingia kwa sheria ambazo zinatoka kwa hii mama ya sheria na hiyo ya dini ya msambwa lakini watu kweli walisema kila mahali watu walisema dini zao. Sasa pia itakuwa majadiliano ya bunge sasa lakini kukiwa na mazungumzo zaidi na hayo kwa mwakilishi wa utamaduni atakuwa J.D. Otiende mazungumze naye. Ile ingine imesema devil worship tuliuliza watu devil worship ni nini. Mwishowe ikatokea watu watakuwa wanaingiliana ati hiyo devil worship wakasema kuna ripoti tukasema hatujawahi kuona hiyo ripoti ya devil worship kama huyo alisema wale wanarandaranda njiani huenda wakasema na wale wanakesha wanasema devil worship wanakutana usiku na wale wanakesha. Halafu wengine wanasema wanafanya meditation na waquarker sasa ni kitu tutajadiliana tuone wengine tukitaka tu kusema worship of the living God sasa sijui kama wahindu wana living God au Wabudhist vitu kama hivyo. sasa hiyo ni mambo imetoka kwa hii iende kwa bunge kujadiliana kutengeza sheria. Hii itapitizwa halafu kule ilenda lakini tutalea hiyo kwa sababu watu wengi walizungumzia devil worship tutasema ilirudia unaelewa Bulima imerudia. Haya tuendelee au hamtaki tufanye hivyo?

**Audience:** Tuendelee

**Com. Adagala:** Mnajua mimi ni mwalimu sasa …(inaudible)…. Tuna vitu vile values nia au lengo lazima hiyo chapter tatu. Lazima taifa iwe na hiyo ili iendelee nafikiri hiyo haiko. Hatuna na lengo, nia kwa sababu mwingereza ndiye alitengeneza hii katiba yetu na ilikuwa tu wacha tuwape wanataka uhuru tunajua ndiyo tunataka. Sasa hivi tumetengeneza ili mimetambua hatuwezi kusoma yote lakini kijana utapeana highlights. Urais hiyo executive na mahakama na legislature na lazima wapate easy goals. Unajua sasa hata ukiambia mtu mambo ya maendeleo ni kutaka kwakke au ukimwambia unafaa tuwe hii nini hapa na pale ni kutaka kwake akitaka. Kuna wabunge wengine hafiki mnalaumu mbunge huyu, wengine wanatuambia salamieni mbunge wetu hatujamuona miaka tano sasa. Wengine wanatuambia mmefanya mzuri kutulea mbunge wetu kwa sababu tumemupigia kura miaka kumi na tano hata hatujui tunapigia nani mnasikia. Sasa sikupenda kwa mtu sasa imekuwa kwa katiba vile tutafuata kila kitu na rais hawezi kufanya vile anapenda nafikiri kazi ingine itatoka kwa directives hizo directives. Hamna nia mbaya lakini akitaka atatoa kama hapendi hatatoa na hiyo ndiyo wanasema kila kitu kiwe chini ya constitution kama national goals.

Umoja na development. What is the development, maendeleo vile vile tuko watu tofauti tofauti na pia itapromote culture, utamaduni, hiyo mambo ya demokrasia itakuwa honestly kitu kizuri sana kwa kiswahlili imepotea kwa kichwa changu transparency, uwazi na wajibu kuwajibika lazima watu watawajibika. Corruption watu walikuwa wanasema zero torelance inasemekana hata sasa hakuna our goal would be zero tolerance. Pengine kesho hatutafaulu lakini itakuwa our goal na ukiona sasa una haki ya kuzungumzia corruption kwa sababu kwa ile katiba nyingin haikuweko sasa unaweza kusema we shall fight corruption. Inasema kwa katiba na ikisema kwa katiba sasa wewe ukisema hivyo unasimama imara na unaweza kuendelea haya

judiciary itakuwa independent mahakama itakuwa na uhuru wake kutokuwa kwa bunge na kwa upande wa urais, hizi political parties kwa katiba sasa inasema lazima wao, sio tu demokrasia ni kupiga kura ya general elections au ya councillors lakini ndani ya party lazima kuwe na demokrasia unajua parties hizi hata ukiangalia ni vigumu kona ipi na ina …sasa ukiwa kwa party ukiwa kwa Safina unaweza kusema hakuna demokrasia hapa tunataka hili na lile ama kuna demokrasia hapa, tunaendeleza hivyo. Kwa manifesto wanaandika hivyo lakini kwa vitendo hakuna hiyo lazima iwe kwa vitendo.

Haya mambo ya NGOs watasaidia pia kwa huo wajibu wa serikali, haki za binadamu ziheshimiwe na kutengenezwa haya hao watu wanawachwa nje nimelalamika kuhusu wao hapa tutakuwa na wakati itakuwa mkutano kama huu hautaendela kwa sababu hapo inasema wanawake lazima wa-participate, people wale walemavu na marginalized watu wako na marginalized kuna sehemu zingine kunaweza kuwa na watu wa tribe nyingine au ethnic group nyingine ndogo mahali kama Nyeri na Wakikuyu lakini sehemu ndogo ina Waturkana nafikiri pia huku Tiriki kuko hivyo kuna sehemu ya Kalenjin okaya hao pia lazima wahusishwe kuna sehemu thelathini ya sehemu zote za kuwakilisha watu itakuwa wanawake, at least 1/3 hiyo ndiyo ya chini lakini inaweza kwenda juu, watoto lazima walindwe na wazazi. Jamuhuri lazima ionyeshe ukweli na haki kwa watu, equitable development inakuja sana watu walilalamikia hii sana na ikawa equitable development sio tu development kwa sehemu moja, sehemu moja ina barabara na North Eastern ina kilometer tatu province nzima ina kilometer tatu ya lami au mahali kwingine kuna maji kuna sitima na mahali kwingine hakuna au kama watu wa Gachoka walikuwa wanasema sitima inatoka kwao lakini hawana sitima pia watu wa Turkwell dam wanasema sitima inatoka kwao hata juna yao na lakini hawana sitima sasa hiyo in equitable development ili watu wote wasitawi kwa usawa na sehemu zote.

Mazingira lazima yalindwe kwa njia ambayo itaendelea kwa …(inaudible)… ingine kwa sasa tu unafikiri mimi nataka makaa nichome nipeleke Dubai au Saudi Arabia halafu unachoma unapeleka lazima ufikirie je na vizazi vingine. Kuna sheria zingine za kimataifa zinatoka UN zinatoka WHO zinatoka the European na serikali lazima zitekeleze. Haya rais atakuwa anareport kwa serikali ile ambayo imetimizwa kwa hizi goals kuna goals na kila mwaka lazima aseme tumetimiza hii na hii na ile bado hii iko nusu na hivyo.

Okay, kuna kitu kinaitwa Mkenya na huyo mwanakenya lazima awe na duties sio freedom peke yake sio uhuru peke yake lakini pia ana wajibu na hiyo iko hapo. Ajue constitution na kuikuza ili itekelezwe hiyo ya kupiga kura hiyo ni duty, msikae nyumbani mnafikiri, Australia ni kuvunja sheria kukosa kupiga kura hata tulizungumzia hiyo lakini tumeweka duty sasa ukikaa nyumbani unavunja duty yako kwa nchi yako kama mwananchi.

Hiyo kila mtu lazima alinde familia yake hiyo ni duty ya citizens. Yes, yani hiyo ni ya community pia for common good sio tu mtu anafanya vile anataka sasa mtu akikosa kulinda familia yake anavunja sheria ya katiba mtu akifanya kitu ambacho kikosana nyumba ya jamii yake hiyo pia ni kuvunja sheria.

Haya, hiyo demokrasia pia inakuja na ukuu wa sheria okay hiyo pia family responsibility iko hapo na family life hiyo tumefanya vibaya hapo? Eeh au tutoe familia hamuelewi sawa public property sasa ni jukumu la kila mtu kulinda. Huwezi kuona kitu kinaharibika halafu unasema, you know sisi tumezoea hiyo lazima ulinde, lazima uone hiki kitu kinaharibika ukilete mbele kiwe

vizuri. Pia mazingira, kila mtu ana jukumu kulinda pia kushirikiana na walindaji wa sheria na kuona vile wanafanya kazi yao na kushirikiana nao. Desist from acts of corruption, hiyo ni… corruption sasa sio unajua wanasema yule anachukua ndio corrupt, yule anapeana pia ni corrupt sasa ni act of corruption. Ukipeana we pia una hatia mbele ya katiba. Ni sasa ni kitu tofauti sana na katiba ni kitu kali ukivunja ni sheria ngumu sana kuelewa ile Kenya inakaa vipi kimataifa. Na hiyo pia wale ambao si Wakenya watu wa raia wa nchi zingine pia hiyo inawahusu swali kwa hiyo hapo tuendelee? tuendelee, pengine nawapeleka pole pole lakini nafikiria wale pia kuna watu wako fast na wengine slow.

Citizenship tulizungumzia sana na tulikuwa na maoni mengi sana kutoka kwa wananchi. Wakenya wote wana haki sawa mbele ya katiba pia jukumu yao ni pia ni sawa wana haki ya Kenya passport na pia ID au unto any others, Ids zingine hapa nafikiri tukisema halafu watu wanaona pengiine ni kitu rahisi hapa kila mtu amezaliwa Mkenya ana haki sawa na mwingne isipokuwa watoto ambao bado wanalindwa lakini yule adult anahaki kama mwingine walemavu wana haki kama wengine wanawake na wanaume haki sawa ndio inatokea hapo hakuna Mkenya, ambaye ako second class citizen wale mko na miaka mnajua tulikuwa second class citizens fourth tulikuwa namba nne Wazungu, wa-Asia halafu wa-Arab halafu sisi hapa kila mtu ako sawa. Kama uko citizen sasa kama uko raia wa Kenya vivyo hivyo constitution mpya ikianza sio tena tutasajilisha watu la! Kama uko citizen sasa unakaa citizen, yule ambaye alikuwa amefanyiwa registration ambaye si mzaliwa pia ataendelea hivyo haya tunapata uraia kwa kuzaliwa, kwa registration yaani unaenda unajisajilisha kuna ile ya kutoka kwa nchi nyingine kuja kwa nchi hii hukuzaliwa hapa. Anyway hiyo citizenship mnaielewa ya kuzaliwa by marriage hii ni muhimu sasa kwa sababu ilikuwa ya mume akioa Mtanzania yule mwanamkwe Mtanzania anakuwa Kenyan citizen, mwanamke akioa Mtanzania yule mwanaume sio citizen, sio raia lakini hapa ni by marriage sasa inaweza kuwa hivyo both ways any Kenyan getting married that person has a right to citizenship anaweza kukataa hiyo ni kitu kingine lakini ana right. Wakivunja ndoa bado hiyo inaendelea. Wale wamekuja nyuma macho yangu si mazuri ndio huyu kijana ananisaidia miaka saba ukikaa Kenya miaka saba na zaidi unaweza kuwa Mwanakenya.

Mtoto akipatikana ndani ya mipaka ya Kenya na miaka nane au zaidi atachukuliwa kama mtoto mzaliwa wa Kenya na tunasema hiyo na sababu kwa sababu vitu vingine huku mbele vina haki za Wanakenya moja yao ikiwa kusema sasa mtoto akionekana ako mtoto ambaye anafaa awe shule na hako shule na wazazi wake hawajulikani unajua watu wengine wanakuja kwa nchi hii kwa njia hiyo hawajulikani au hawaonekani sasa atachukuliwa kuwa Mkenya ili aende shule. Na pia matibabu na vitu kama hivyo …(inaudible)… adopted yule ambaye akifika miaka kumi na nane ana right ana haki anaweza kukataa, lakini ana haki ya kuwa citizen kama si mzaliwa wa Kenya. Kuna citizenship mara mbili kuna sasa ukiwa citizen wa Kenya akaenda Zimbabwe sababu wakamwambia chagua sasa akachagua ya Zimbabwe lakini Kenya pia inasema utachagua sasa akachagua kuwa kule lakini sasa kama mtoto wake ana shida ni story ndefu lakini mtu anaweza kuwa citizen wa nchi mbili na tuona Wakenya particularly, hii dot com wanaendelea sana na wanafanya kazi kila mahali awe na citizenship ya Kenya na pia ya nchi ili ingine kama inaruhusu. Germany ukienda huwezi kuwa citizen wa Germany na pia Wakenya na unajua hiyo shida lakini Kenya itakuruhusu.

Ukipoteza uraia wako unawacha ku-apply tena. Kama umechukua uraia kwa njia ya magendo na sio njia halali inaweza

kupokonywa hiyo serikali inaweza kunyang'anywa hiyo uraia. Na mnajua hapa Kenya kuna biashara ya njia hiyo sasa hiyo watangaangalia waone huyu alikuwaje citizen kuzuliwa hiyo ni haki yako hiyo tumesema hivyo…(inaudible)…. Sasa hii ingine ukipata kwa njia ya magendo inaweza kutolewa. Haya tena hiyo ya wazazi kufa na wazazi pia hiyo ina sheria yake hapo kama anazaliwa Kenya lakini wazazi si Wakenya au amezaliwa nje na wazazi wake ni Wakenya. Kuna ingine ya kuishi resident ni kama huyu walikuwa citizen wa zamani na mwanamke au mume wa ndoa wa nchi ingine anaweza kuwa resident citizen lakini hapa ni resident na mtoto wa citizen anaweza kuwa …(inaudible)…. Parliament itatoa one year, lazima watengeneze hayo yote. Vile inafaa mtu awe mwana raia mwanakenya vile kuchukua ile kazi ya parliament vile watu watapata uraia hiyo application hiyo ya kutupa mbali uraia wa Kenya kama mtu anataka kukana na kutupa mbali tuakua na sheria pia. Kunyang'anywa hiyo citizenship, …(inaudible)… kutakuwa na registration board ya almashauri ya uraia. Swali hapo? Tuendelee uraia, tutaenda haraka haraka sasa hapa nafikiri…

**Interjection:** Ningekuuliza swali lakini kwa sababu umenikataza wacha tu.

**Com. Adagala:** No ukiwa kwa uraia unajaua unauliza kama …(inaudible)…

**Avedi Bulira:** Mimi nimeona hapa hiyo citizenship. Avedi Bulira, nafikiria hapa tumefanya makosa you are either a Kenyan or not a Kenyan. Hii tunaweka kwa constitution ku-protect hawa Wahindi wanakuja hapa kunyakua mali yetu wanajiita Wakenya na mguu mwingine uko huko Ulaya. Akisha shiba anabeba mali yote anapeleka Ulaya sasa anasema mimi si Mkenya mimi nataka tutoe hiyo tuseme either you are a Kenyan or you are not a Kenyan hawa wakiwa hapa tujue they are foreigners they are expartriates tunawakubalia kukaa na sisi.

**Com. Adagala:** Citizenship pia ina upande mwingine. Wewe mzee mtoto wako akienda France anaolewa huko unaelewa mzee. Ana haki ya kuwa Kenyan? Wakike au wakiume kwa sababu saa zingine unaishi mahali halafu anakuambia amua na una kazi hapo na anakimbia amua utaishi kama citizen au la?

**Bulira:** Akizaliwa huko anakuwa citizenship wa huko.

**Com. Adagala:** Pia mwanamume tena mwanamke peke yake hakuna ubaguzi kwa katiba na pia kulikuwa na mzee mwingine alizaa wasichana peke yake na hao wasichana wote hata ni mluyha wameolewa nje sasa hivyo mzee aliona sasa hakuna mjukuu wangu hata mmoja atakuwa Mkenya ni kama laini yake imekwisha kwa Kenya. Mnaelewa so pia nataka watu waelewe hii si maoni ya commission hii ni maoni ya wananchi wengi walisema na pia kuna watu wanaishi wadogo wako kwa mpaka wa Tanzania Waturkana wako kwa mpaka wa Sudan na Ethiopia na Uganda na wanasema unaweza kuoa mwanamke au uolewe na umalize miaka thelathini hata hauna ndoa kwa sababu huyu mtu hawezi kuwa Mkenya unaona hiyo kuna watu wa mipaka pia raia wa kawaida tu unajua sehemu ya juu ya …(inaudible)…. Na hiyo ingine na kuna hii ya dini na pia kina hiyo nyingine ya wale wako hapa kama Wahindi kuwa hapa na huwa pia hiyo lakini unajua vitu vya katiba ni vitu unavitoa kwa moyo na pia ukiwa na nini zaidi kama ukiwa Somalia na sasa unaona vitu vyote unaenda sasa pia unaweza kuwa hapo ya what did I call it? Hiyo ya ku-terminate citizenship kwa sababu itakuwa kama umekosea nchi. Haya tuendelee …(inaudible)…. Tries to be for the

common good, for the great number.

**Ben Chemange:** Jina yangu ni Ben Chemange kwa upande wa citizenship and marriage hapo ninaona kwa maoni yangu naona si mzuri mtu kukaa hapa ….(inaudible)… mtu kukaa Kenya miaka tatu na hapa mimi naona kama anaoa citizenship under marriage. Sasa situtajaza wakora wengi hapa kutoka Tanzania, kutoka Uganda, Somali wakija hapa wanaoa wasichana wetu na hawa watu ni …(inaudible)… kwa maana miaka tatu ni kidogo sana. pendekezo langu ingekuwa kama miaka kumi kwenda mbele.

**Com. Adagala:** Asante sana kwa hilo pendekezo la pili tunafungua, lakini tufikirie pia watoto wetu wengi wako kwa nchi zingine tufikirie hapo na pia wao ndio wamesema I lost my Kenyan citizenship na si wanaleta pesa they send $20 you look like you are, send you $100 mnakula kitu haya tuendelee lakini tumeweka hilo pendekezo kutoka kwa mzee Bill of RIghts. Hapa nido tunao ile inaitwa ukatiba tunaweka vipi ukatiba ili inakuwa maisha na sio kitabu unajua hii katiba ingine tunayo ni kitabu na ukivunja sheria ndio unajua kuna katiba au kuna sheria lakini tunataka iwe zaidi ya makaratasi.

**Watako:** Katiba hii itakuwa katika imejengwa kwa nguzo za demokrasia na haswa katiba hii katika haki za binadamu imepeana haki kama haki ya maisha.

**Com. Adagala:** Right to life

**Watako:** Equality ama usawa

**Com. Adagala:** Usawa

**Watako:** Uhuru kutokana na discrimination ama kubaguana wanawake pia wamepewa haki

**Com. Adagala:** Kubagua sio serikali pekee ndio inabagua au usawa tuatingia kwa maisha vile tunakaa, vile tunashirikiana upande wa kazi, upande wa nyumbani, upande wa kanisa, upande hayo mambo sasa hii ndio inaingia to line with constitutionalism sasa hiyo philosophia inakuwa ndio philosophia ya maisha hiyo ndiyo inaingia.

**Watako:** Wanawake pia wamepewa haki katika haki hizi wazee pia wametambuliwa katika katiba. Katiba inasema kwamba watapewa uwezo wa ku-participate kushiriki katika maswala ya jamii, pia wataruhusiwa kufanya mambo yao, pia watakuwa huru ama watakuwa autonomous, watoto pia wamepewa haki katika katiba, haki ya kulindwa, kuwa na jina, kuwa na nationality ama kuwa Wanakenya, wako na haki ya kutunzwa na wazazi ama parental care watapewa elimu, elimu sasa ni haki, hawatabaguliwa, kupewa chakula, education hawatapigwa viboko shuleni, corporal punishment imetolewa, hawatafungwa na kufungwa pamoja na wale wahalifu katika jela, watapewa jela zao tofauti pia.

**Com. Adagala:** Hiyo iko kwa Act kwa Children’s Act 2001 sasa hiyo ilikuwa kama ile tuwe kwa katiba hii. Nafikiri mumeona kuna bills nyingi zinakuja kwa parliament na wanapitisha au wana na inaambatana hapa hiyo ya 2001 Children’s Act.

**Watako:** Familia pia imeangaliwa katika katiba sasa ni haki kwa mtu yeyote kuanzisha familia yake na familia pia imetunzwa, marriages ama ndoa pia zimetunzwa kuna ndoa tofauti zitatunzwa na katiba na sheria zingine ambazo bunge itapitisha watu walemavu pia wamepewa kipa umbele hapa, wako na haki ya kuelemishwa, ya kuvunja na institutions ama institutions za disabled pia itakuwa haki kwao kufunzwa lugha za kitaifa pia hapa parliament pia imepewa uwezo wa kupitisha na kutoa masharti ya kusaidia hawa watu walemavu.

**Com. Adagala:** Kuna ingine inaitwa human dignity sijui kama kuna mwalimu wa kiswahili haijatoka tafsiri lakini kuna kitu human dignity and the right to have that dignity respected and protected. Sasa katiba ni kitu cha ajabu sehemu ndogo kama hiyo ina nguvu nyingi sana sasa kwa matatu hakuna mtu kukupanga kwa matatu kama wewe ni gunia au ni sponge, mnaelewa? Hakuna mambo ya mtu kumtusi mwingine bila sababu atakuwa amevunja sheria kuna vitu vingi sana hapa dignity hata hiyo nyingine inaingia ya nguo na chakula na elimu inaingia tu kwa hiyo shemu ndogo dignity mtu kuheshimiwa kila mtu ana haki kuheshimiwa.

**Watako:** Pia katiba inatambua haki ya ulinzi kila Mwanakenya sasa ako na haki ya ulinzi na sasa katika haki hii ile kubaguliwa, fujo dhidi ya mwanadamu inatupiliwa mbali pia katika kuna haki, haki, freedom from slavery and haki ya utumwa, kutokuwa mtumwa. Sasa hakuna mwanakenya ambaye atalazimishwa kufanya kazi bila malipo pia kila mwanakenya ana haki ya privacy, usiri uko na haki ya kuwa na siri siri zako za kibinafsi na hata siri ya nyumbani hakuna ile inatendeka mara nyingin utaona poliis wanakuja wanakuvuruga huko nyumbani wanataka sijui nini sasa hii ni kinyume ya katiba pia kuna haki ya kuabudu hii tumeongea juu yake freedom of worship and opinion. Pia kutakuwa na haki ya public opinion, kutakuwa on national issues maswala ya kimataifa na kitaifa kila mwanakenya atakuwa na ile haki ya kuwa na rai yake, opinion yako uko na haki kwa swala lolote la kitaifa na la kimataifa pia ni haki sasa ya kupata information kutoka kwa serikali.

**Com. Adagala:** Hiyo haki ya kutoa maoni ni vile imekuwa mbele ya tume hii. Sio kusema tulikuwa tumeshasema wewe umesema nini lazima kila mtu aseme na kila mtu achange kwa mjadala kama wa taifa na hakuna mtu kuzungumzia mwingine bila kuchaguliwa yule amechagua ukichagua mtu unampa ruhusa ya kukuzungumzia lakini pia bado una hiyo haki.

**Watako:** Pia kuna haki ya assembly. Mnaweza kusanyika kidini bila kufurugwa na polisi pia uko na haki ya kusimama katika ya kupiga kura na pia kusimama katika uchaguzi wa kitaifa, kuna haki ya kutembea sehemu yoyote ya Kenya, haki hii lakini imepunguzwa kwa wasio wakenya wale refugees wao watakuwa na confined areas, pia kutakuwa na haki ya kufanya kazi, kazi yako, freedom of trade, occupation and profession utafanya kazi yako bila kusumbuliwa, utakuwa na haki ya kulinda mali yako lakini kwa sasa katiba hii inasema kwamba watu ambao wamepata mali kwa njia isiyo halali hiyo mali haitalindwa na katiba lakini watu waliopata mali kwa njia iliyo halali mali hiyo italindwa na katiba.

**Com. Adagala:** Kama hiyo ya watu, hawkers, hao jua kali kuna haki ya kutengeneza kazi yako unajua kama kule Nairobi unakimbizwa huku na kule lakini kwa sheria, chini ya sheria kuna haki ya kujitekeleza lakini huwezi pia kuvunja sheria.

**Watako:** Katiba imeangalia kazi ya haki ya mfanyikazi. Kila mfanyikazi anawezajiunga na chama kinachowakilisha maslahi ya

wafanyikazi kama waalimu wako na KNUT sasa hiyo ni haki ambayo iko katika katiba. Pia retirement wenye wame-retire social security pia ni haki hawa watu wanastahili kutunzwa kupata assistance kutoka kwa government. Afya, elimu, mambo ya housing ama nyumba, chakula, maji, sanitation ama usafi na zile haki za kimsingi basic needs sasa ni haki ambayo iko katika katiba, katiba hii pia itatunza lugha za kitamaduni na culture, consumers ama wale ambao tunanunua vitu kila Mkenya ni consumer pia sasa hizi unalindwa katika katiba saa zingine unaenda dukani unanunua kitu ambacho hakifanya kazi sasa katika katiba hii unalindwa una haki unaponunua kitu au unapopata service lazima hiyo service upate manufaa ya pesa zako pia kila mwanakenya atanufaika na administration, utanufaika na uongozi amabo ni wa manufaa hakuna mwanakenya ambaye atahitajika kukubali masharti ama instructions ambazo si za halali hii haki ni ya watu wako katika kikosi cha polisi na wanajeshi. Wakipewa unlawful instructions wanaweza kataa. Pia kila mwanakenya atakuwa na haki ya kufika kotini kama ako na kesi.

**Com. Adagala:** Hata hapo ya instructions, ni kama hivyo mtu yuko kazini, anakwambia higher authority bila kusema ni nani ama ni sheria gani inakulazimisha. Unajua hiyo kitu kinaendelea sana au unaambiwa tu lazima ufanye sasa hiyo ni kitu ambacho wananchi wamekingwa hapo.

**Watako:** Wananchi hawatakuwa wananyanyaswa na polisi uko na haki ya kutonyanyaswa na polisi wakati unashikwa na unaposhikwa una haki ya kupata trial ambayo ni fair. Unapofika kotini lazima upewe muda wa kujitayarisha, lazima kesi yako isikizwe mahakamani. Pia watu ambao wako kwa cell za polisi wako na haki watapewa ile privacy wanaweza kuwasiliana na watu wengine kama mawakili ama familia halafu pia wananchi wana haki wakati wa emergency wakati serikali inatangaza hali ya hatari kuna haki fulani ambazo serikali itabidi zikiueke, haki za kimsingi kama kunyanyaswa kwa wananchi ambao wasio na hatia na sasa korti ama mahakama zimepewa haki ya ku-interprete ama kutafsiri hizi haki uwezo umepewa mahakama na pia kuna tume ambao zimebuniwa katika katiba kuna tume ya kahi kuangalia kwamba haki za binadamu, haki za wananchi zinafuatwa katika bali na tume hiyo kuna watu ambao hawawezi labda kulipa wakili wawakilishe kotini, kuna ofisi ambayo imebuniwa katika katiba ambayo itasaidia wale watu ambao wasiojiweza mahakamani watapata hiyo legal aid.

**Com. Adagala:** …(inaudible)… ulituuliza kwa sababu mawakili wana bei ya juu sana sivyo? Ukatuuliza kunaweza kuwa na mtu akienda kortini awakilishwe na serikali ilipe huyo mtu tumeweka hapo hivyo?

**Watako:** …(inaudible)….nilitaka kusema hizo haki zingine ziko hapo ya afya, ya elimu, ya compulsory primary education mtazisoma lakini hizi ni vitu wananchi waliuliza kwanza ni pages …(inaudible)… sasa ubaya wa mambo haya ni kwa vile tumeyasikia siku nyingi lakini inasemekana halafu for instaance watu wakisema hasa primary education iwe compulsory sas nilikuwa nauliza wamama wengine utapata siku moja hulipi fees ya primary utajua ilioteka age na ushiriki kwa katiba. Sasa wale walitoa ndiyo wameleta hii free primary education na hiyo mambo ingine hata ya maji-watu wengine wametuambia hii ni ndoto lakini kwa vile inasemekana na hasa wanasiasa halafu inakuwa kama election halafu inapotea au wanachanganyikiwa hao mbele mmoja anasema hivi mwingine hivyo lakini sasa itakuwa lazima itimizwe kwa sababu iko kwa katiba. Hata mbeleni haikuweko ilikuwa tu kitu cha kusema kama directive au mdomo hata imeandikwa kama policy lakini haiwezi kuendelea sasa kama haiko kwa katiba. Tulikuwa na mzee alikuwa na swali ya wazee wakongwe alikuwa mzee mgani? Alikuwa ni wewe? Wazee, Kegode

ameenda …(inaudible)…

**Nahashon Kegode:** Jina ni Nahashon Kegode. Nilikuwa nasema wazee wakongwe na wamama wakongwe. Mama mkongwe amefiwa na mume wake…

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Kegode:** Ningependa wao katika katiba wanaweza kuhudumiwa. Ningependa katiba iwaweke chini na wazee kama wale wame-retire ni kitu gani kinawafanya warudi kule waliko taabu. Pendekezo ni kwamba mzee aki-retire yeye na party yake apewe pesa zake afanye kazi yake na pahali alipotoka kijana arudi afanye kazi hiyo.

**Com. Adagala:** Hata kama kijana amesoma amefika university na mzee alikuwa watchman, unajua vitu vingine hivyo viko ndani. Hiyo social security na welfare ya elderly iko. Ukipata ile ya kiswahili utaona iko unasikia mzee, iko ndani wazee walilamika sana na tumewekwa wakongwe wa katiba, wapate hata hiyo pension walisema mtu akifariki mjane wake au mtu mwenyewe mwanaume wake apate pension mpaka maisha. Sas hiyo itatengenezwa kwa sheria lakini tutaendelea. Tafadhali …(inaudible)…

**Juma Noor:** Mimi naitwa Juma Noor. Swali langu lilikuwa ni kuhusiana na rights na katika hii right yenyewe nazungumzia habari ya mahakama kuna wakati mtu anatendewa swali na inakuwa kwamba lazima ukienda mahakamani uwe na mashahidi wawili. Sasa mimi nilikuwa niki-propose ya kwamba tofauti na mashahidi wawili hata huyu shahidi mmoja aliyepatikana ingelikuwa ni vizuri korti ikubaliane naye kuweza swala hilo bila shahidi wa pili kwa sababu watu wengi wanaogopa kwenda mahakamani.

**Com. Adagala:** Wakili anasema hakuna kitu kama hicho lazima uwe na shahidi wawili. Pengine inasemekana kwa korti lakini kwa sheria haiko. Ikiwa mkono uwe umefika hapa tafadhali harakisheni. Hii bill of rights tulizungumzia Jumapili kuna mtu ambaye ameisikia kwa kingereza Prof. Ghai akizungumzia nani alisikiliza please tune in msiwachwe nyuma. Jumapili saa tisa ilikuweko tena ile Jumapili ingine itakuweko tunajaribu kuwe iwe saa tano hadi saa saba na saa nane hadi saa kumi tafadhali. Sikizeni hiyo majadiliano ili muerevuke.

**Arthur Kadendi:** Jina ni Arthur Kadendi. Saa mimi nimchagua mbunge namwita mheshimiwa. Nikimwita mheshimiwa je naye aniite nini?

**Com. Adagala:** Nafikiri nyote ni raia.

**Thomas Kibiende:** Mimi kwa jina ni Thomas Kibiende. Napendekeza ningesimamia kwa hii rights ya watoto. kama mtoto anafaa kusomeshwa na mzazi, sasa upande wa masomo unawezakuta baba ana …

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Kibiende:** pendekezo ningependa mtoto asome sasa napenda masomo yawe free kwa watoto.

**Malecha Ngusanya:** Kwa jina naitwa Malecha Ngusanya. Mimi nikuuliza kuhusu hawa mahakimu. Ningependa mahakimu kama inawezekana kwa sababu wamepata cancer ile kidogo ya kupata rushwa ingefaa watafute watu wengine wapya wapate nafasi.

**Com. Adagala:** Nafikiri uwe unasikiliza. Kuna kitu kinaitwa zero tolerance for corruption. Na hiyo itakuwa kitu kali *khuli omunyu kobukere saru.* Usikii, usikilize ndiyo unauliza maserahi ambayo imepetishwa. Kijana huyu jina lake nani? Meshack usikilize ndivyo nauliza maswali ambayo tulimaliza juu. Hakuna rushwa na pia hao wengine wote hivyo ndivyo unaona wanatupeleka kotini. Wakina mama tafadhali songeni sitaki hii mambo yenu sitaki kabisa. Tabia mumetengeneza ndiyo unamfanya hiyo inakufanya sikilizeni wewe unavaa hii yello ribbon ni kwa sababu judges hawakutaka wachunguzwe walitajirika vipi walifanya kesi vipi hivyo ndiyo mnaelewa. Meshack umeelewa ama umepotea kwa soda? Hiyo pia itakuweko na wale wako na record mbaya mko hapo kwa sehemu ya judiciary una katiba wewe Meshack kweli umepata? Utasema. Msiulize maswali kiholela tu tunaomba kwa utaratibu. Wengine wanarukaruka, tukirukaruka hivyo hatutamaliza lakini tunajibu tu kwa sababu …(inaudible)…

**Watako:** Sasa ni sura ya sita ambayo inahusu wakilishi representation of the people. Katiba ..

**Com. Adagala:** Excuse me please stay outside with your mobile unaharibu record yetu. Zima kila mobile give it one day in fifty. Kama biashara inaungua ama girlfriend amekua vipi tafadhali vumilia.

**Watako:** Kuhusu uwakilishaji wa katiba imetoa mwongozo na muongozo, huu ni kwamba upigaji wa kura utakuwa wa kisiri au secret ballot. Hakutakuwa na maneno ya mlolongo tena na kura zitakuwa za free and fair huru na haki. Na katika kura katiba ina mwongozo kuhusu wanawake kwamba katika uchaguzi lazima wanawake pia wa-take part ama wa-participate. Na uchaguzi utatendeka bila interference kutoka kwa serikali. katiba hii pia anapatia wabunge uwezo wa kupitisha sheria kuhusu nomination ama uteuzi wa mambo ya usajili wa ukubwa wapiga kura utakuwa unaendelea continuous. Halafu kila mwanakenya ako na haki ya kupiga kura pia kila mwanakenya ambaye ako na miaka kumi na nane anaishi hapa Kenya ama he is a resident here atakuwa na haki ya kusajiliwa na kupiga kura. Lakini mtu ambaye hana akili timamu hataruhusiwa kupiga kura ama atakuwa disqualified. Mtu ambaye alikuwa mwanakenya lakini amepoteza uwanakenya wake. Tume ya uchaguzi pia imebuniwa katika katiba. Watu wa commission wa tume…

**Com. Adagala:** Hiyo ya kusema sisi unafikiri pengine tukiketi hapa haki ya Kenya katikati ya Kenya middle of Kenya tunaona si kitu lakini huko mpakani mtu anaenda leta lori ya watu 600 kutoka Uganda au kutoka Tanzania kwa sababu hawezi kutambulika ni Wadigo kama Wadigo wengine. sasa hiyo haitattekeleza na ingine tu huwezi kukua hapa na wewe si raia, citizen na upige kura.

**Watako:** Pia qualification ya kazi ya hawa ma-commissioners imeandikwa katika katiba pia kila mwanakenya ako na haki ya

kubuni chama cha kisiasa. Right to form a political party, pia sasa ni haki katika katiba. Halafu kazi ya hizo political parties imeandikwa katika katiba ni vipi vyama vya kisiasa vitakuwa vinafanya jinsi watakavyo pata fedha zao. Usajili wa political parties ama vyama vya kisiasa vitakuwa huru kufanya kazi yao bila kusumbuliwa na serikali ambayo inatawala wakati huo, serikali vyama vya kisiasa pia vitapata fedha kutoka kwa serikali lakini havitaruhusiwa kupata fedha kutoka kwa serikali lakini havitaruhusiwa kupata fedha kutoka kwa nchi za nje. Katiba hii hairuhusu watu ambao sio wakenya kuleta pesa zao katika vyama vya kisiasa ili kufunga nchi. Pia tume ya uchaguzi itakuwa na haki ya cancel ikisajili mtu itakuwa na haki ya ku-restock hiyo registration ikiwa hivyo mtu labda hakuwa mwanakenya ama aligeuka taratibu za usajili. Vyama vya kisiasa vitakuwa na fedha ambazo zitatengwa, fund iko established under constitution. Pia vyama vya kisiasa vitaongozwa kuna mwongozo ambao uko katika katiba vitaongozwa na tume ya uchaguzi ambayo utakuwa inasajili hiyo vyama na pia itakuwa inakadiri kuona vile vyama vya kisiasa vinaendelea na kazi zao.

Party discipline, mkaguzi wa vyama vya kisiasa na pia the conduct ya political parties iko ndani ya katiba. Rais pia hatakubaliwa kuwa mwanachama au kuwa na afisi katika chama. Saa hizi utaona kwamba president wa chama labda ama chairman wa chama ndiye anasimamia ama anagombea katika chama hicho lakini kwa sasa katika mwongozo huo wa katiba mtu ambaye ni rais hatakuwa hatashika nchi katika chama chochote cha kisiasa tunataka uhuru hatutaki mapendeleo. Tume ya uchaguzi imebuniwa katika katiba ni tume hii ambayo itakuwa inasajili vyama vya siasa. Saa hizi vyama vya kisiasa vinasajiliwa na afisi ya mkuu wa sheria lakini saa hizi katika katiba hii vyama vya kisiasa vitakuwa vinasajiliwa na tume ya uchaguzi nasema kwamba katiba hii imetoa qualifications za ma-commissioners wa tume idadi yao na pia tume ya uchaguzi ifayakuwa shughuli na functions za vyama vya kisiasa.

**Com. Adagala:** Tume vile mnajua tume yetu ya ECK ni moja duniani ambayo iko kubwa sana. Iko 22 members na hiyo ni kubwa sana unafikiri kuna wengine wako maximum ten, na zingine ni mtu mmoja na ma-assistant wake. Tena hapo watakuwa watu wanane kati ya watu wanane na zaidi watu kumi hiyo ndiyo itakuwa inasajili vyama.

Political parties are registered with ECK mnaelewa sasa haitakuweko kwa sababu political parties unajua saa zingine wanasema ni NGO's sasa ziwe political party itasajiliwa na ECK. Kuna chairperson and other members of the commission shall be appointed by the president with the approval of the national assembly mnaelewa hapo? Yes, watakuwa appointed. Musome hiyo ili mjue kwa sababu haya ni mambo yatatekelezwa, we have a schedule for that. Tume hii iko, itakuwa in office for the purposes of the election hivyo iko kwa schedule. Schedule yenyewe iko wapi? They would be in office for 90 days, please read the schedule that goes with the electoral commission.

After the election the present ECK will be disbanded and a new one with the rules under the constitution will be elected. It is very important. Our 8th schedule hiyo ya nane nikiangilia nyuma mtaona 8th schedule wengine ninataka sana nijue details. Details ziko kwa schedule vipi itatkelezwa. Nataka kusema tu ili ijulikane hivi itume iko tu kwa wakati wa transition. Conduct the forth coming election be in office to wind up this business 90 days inatakiwa na hapo parliament itakuweko na president atakuweko, national assembly itakuweko na wataunda ingine. Hiyo tu kwa hayo any question from that one. Any question political party

…(inaudible)…

**Ndolo Asava:** Naitwa Ndolo Asava. Hapa kwa matumizi ya hela kwa political parties sijui lakini kwenye tumefika sijaona kama kuna regulation yenye itaelekezaa jinsi yenye wale ambao wako ndani ya chama fulani watatumia hela zao na jinsi watakavyopata zile hela au wanaruhusiwa kupata popote na kutumia kupata popote na kutumia jinsi unavyotaka kama hapa if you are an independent candidate.

**Com. Adagala:** We read schedule eight, please it has many details even concerning the parties which would have not be registered by a certain period what will happen to their MPs independent …(inaudible)… read schedule eight kuna many details we discussed all those but they are many details we discusssssed all those but they are many details. Please read that. Nani swali nzuri hata hivyo but note that issue.

**Shem Otiende Susa:** Kwa majina ni Shem Otiende Sisa. Nauliza kwa wale ambao wanawania viti aidha social authority au parliamentary what qualifications should they have.

**Com. Adagala:** Because wananchi had a lot of maoni on that itakuja kwa representation

**Onzere Oberi:** Pendekezo, Onzere Oberi, natoa pendekezo ningependa tuwe na vyama vitatu tu, ama viwili vya kisiasa ambavyo vitasajiliwa na serikali yetu.

**Com. Adagala:** Pendekezo hilo litakuweko nafikiri tulichukua vile tulichukua makanisa. It is limitation of association na limitation of expression na hiyo ikitoa basi umeweka bomb kwa katiba. Kuna vitu vingine ambavyo vinaitwa misingi ya katiba na hiyo ni moja yao. Sasa kweli tulijadiliana sana na tukasema hiyo itakuwa self regulating kujisajilisha kuwa na wabunge kwa bunge kwa local authority hiyo ndiyo itaonyesha mwenendo yao ndiyo itaonyesha hiki ni chama na wana responsibilities hata development. Na vile watu wameanza kama mergers na hii unaona NAK has many parties in it eight. You see hiyo sasa ni self regulating unaona hatuna nguvu tutakazwa au kamao uko chama na hauna mbunge kwa bunge hiyo pia itaenda kwa ECK waseme hiki ni chama cha aina gani na vitu kama hivyo. Ukiwa na chama na Rais wenu atachukua tu province mbili pia kuna limitation hapo ambayo inasema five provinces hiyo tu-retain that one five provinces. So we have other types of regulations. So if your presinde even if he wins elections and Central, Nyanza and Western has the most votes he can be president. Then they will be a run off so that he gets five provinces was it 30%, 20% I think they reduced it. Unaona hiyo lakini you cannot limit freedom of association.

**Anne Khaiga:** Kwa majina naitwa Anne Khaiga. Swali langu ni kwamba shida ya wamama kuingia kwa bunge pesa nyingi ni watu ambao wanataka kuchaguliwa wanatumia pesa nyingi. Hatujui katika itasaidia aje wamama ambao wanatoka kupigania hizi viti.

**Com. Adagala:** Nimefurahia sana umesema kupigania. Kwenda bunge ni kupigania lakini hii tutazungumzia inakuja lakini kwa parties pia parties must show that right ya wanaweka, walemavu, youth tuseme hamuwezi tu kusema chama cha nini hata kuna

hiyo funding inatoka kwa serikali inaambatana na mambo hayo. Mtasoma mutaona inaambatana na mambo hayo wakina mama msome kuna kitu kinaitwa cross cutting issues na mumeona mambo ya akina maina imekuja kwa citizenship, equal rights, parties, bunge. Mambo ya wanawake si bunge peke yake imekuja kwa familia in cross cutting issue iko kwa isssues zote sasa mama utasikiliza uwache mambo ya serving uketi usikilize na mimi sipendi hii mambo ya akina mama hii ni utumwa. Na utumwa umekatazwa hapa …(inaudible)….

**Watako:** Rais atakuwa na mamlaka ya kuwateuwa ma-commissioners wa commissions of inquiry kama ilivyo sasa. Rais pia ataona kwamba, ama atakuwa na juhudi ya kuona kwamba serikali inaambatana na international instruments ama mikataba ya kimataifa. Rais pia atakuwa na mamlaka ya ku-declare war ama hali ya hatari atakuwa na mamlaka ya kusema kwamba saa hizi tuko kwa hali ya hatari na pia atakuwa na uwezo wa kuwasamehe wanalokosa wale ambao wamepitia kwa mahakama hatia rais atakuwa na uwezo wa kuwasamehea. Rais atakuwa na uwezo wa kupata rai ya bunge kuhusu maswala fulani ya sheria ama kuiambia bunge ipitishe sheria ama kuiambia bunge ipitishe sheria fulani fulani inapohitajika.

Atakuwa pia na uwezo wa kutia sahihi katiba sheria ambazo zimepitishwa na bunge ama the power of assent ingawaje bunge pia itakuwa na uwezo wa ku-overide hi power of assent. Katiba hii pia imeweka taratibu ama calendar ambapo uchaguzi wa rais utafanywa. Kwanza rais atatumikia katika vipindi viwili vya miaka mitano. Two terms of five years lakini baada ya term ya rais uchaguzi utafanywa jumanne ya kwanza ya mwezi wa nane but baada ya kipindi cha rais. Kipindi cha rais kikiisha cha miaka mitano, kikiisha kutakuwa na uchaguzi huu utakuwa siku ya jumanne wa mwezi Agosti.

**Com. Adagala:** watu wengi walisema wanataka calenda wajue siku fulani ni ya kupiga kura kwa rais. Therefore ni kitu tumewekewa kwa sababu wananchi walisema hii kitu inabadilika 1988 was in March, 1983 something like that then November, December okay. Pia mswada huu uko na qualifications ama vitu ambavyo rais atatakikana atimize na kitu cha kwanza lazima awe Mkenya, lazima awe na miaka thelathini na tano na juu, awe mtu msitawiki awe a person of moral intergrity, awe na shahada ya degree kutoka university ama chuo kikuu ambacho kinatambulika, awe amependekezwa na chama cha siasa ambacho kimesajiliwa. Ama awe independent candidate lakini lazima atimize sharti fulani, lazima awe na kura ama lazima awe na sahihi elfu moja za watu ambao wame-register as voters. Katika kila mkoa in each province lazima awe na watu sahihi elfu moja, lakini mtu ambaye sio Mkenya ama ambaye amechukua kiapo cha kuitumikia nchi fulani mtu huyo hatakubaliwa kuwa rais. Huo utaratibu wa kura.

**Com. Adagala:** Hilo jambo la Mkenya tulijadiliana lakini mwishowe tuliweka tu mwanakenya lakini memo na kuwa njia nyingi ya kuwa mwanakenya. Sasa mimi naweza kwenda na Gachoka nimependa sana halafu nimeona nikumuona alikokuwa?

**Interjection:** Mkenya

**Com. Adagala:** Na ana pesa anaweza kukaa miaka tano hivi halafu aseme anataka kusimama. Sijui ningefikia hapo sasa ni hilo pendekezo lenu hivi vita namwambia tulijadiliana inafaa ije mgeuze iwe kama unakubali lakini tuliona inafaa iwe mzaliwa wa Kenya. Infact huyu mtu anaitwa he is a black American lazima wazazi wake wawe citizen ndiyo wewe uwe na hiyo kuwa rais. Lakini mimi niliona hapa unaweza kuwa rais lakini inafaa mfikirie na mpe hawa wawakilishi wenu au mtu kama anapendekeza sasa lakini hiyo ya kusema mhindi anaweza kutoka India na ten years later he is president unaona hiyo.

**Watako:** Hii katiba inatoa mwongozo wa uchaguzi hiyo tunasema pia rais atatumikia vipindi viwili vya miaka kumi na tano na iwapo kuna tashwishi kuhusu uchaguzi wa rais korti ya juu zaidi ambayo itakuwa supreme court, ndiyo itakuwa na uwezo wa kisikiza petitions.

**Com. Adagala:** Sasa hapo mmesikia, supreme court. Namusikie kwa sababu tutazungumzia kwa next chapter.

**Watako:** Rais anaweza kutolewa na bunge kwa impeachment. Sasa rais huyu itakuwa inawezekana kwa rais ambaye unaona labda amefanya makosa fulani, bunge inaweza kumshtaki ama kum-impeach na ikiwa atapatikana na hati atatolewa na iwapo rais anatoka makamu wa rais atakuwa kwa ofisi atashikilia wadhifa wa rais kwa muda fulani. Mliambiwa kwamba vice president lazima atakuwa running mate wa president. Mamlaka ya vice president ama vice president, atachaguliwa chini ya sheria za electoral commission ama electoral commission ndiyo itatekeleza uchaguzi wa vice president. Kazi za vice president functions wajibu wake pia umeandikwa katika katiba atamsaidia rais katika kazi yake na atafanya kazi ile ingine ambayo sheria itampa na hatashikilia ofisi ingine katika uma vile ile ya makamu wa rais.

Mshahara wa rais na wa makamu wa rais utajadiliwa ama utatengwa na tume ya mishahara ambayo iko ndani ya constitution, remuneration commission. Tume hii pia ndiyo itakayo jadili na kupitisha mishahara ya bunge. Pia katiba hii imeleta afisi ya prime minister ama waziri mkuu. Waziri mkuu atateuliwa katika chama kilicho na viti vingi zaidi bungeni na iwapo katika chama ambacho kuna viti vingi zaidi bungeni kutampata mtu ambaye anaweza kuunga mkono na majority na wabunge wengi zaidi ama atatolewa na wabunge through a vote of no confidence ama kura ya kutokuwa na imani.

Mtu yeyote ama mbunge ambaye anawakilisha chama kilicho na wanachama wachache atateuliwa kwa waziri mkuu. Masharti haya yote yako katika kifungu cha mia moja sabini na moja mtajisomea hayo. Na pia waziri mkuu anaweza kupoteza ofisi yake iwapo ataamua kujiuzulu ama iwapo bunge itapitisha kura ya kutokuwa na imani naye. Tumesema hapo awali kwamba kutakuwa na mawaziri kumi na watano na wasaidizi wake wao kumi na tano ambao mawaziri hatakuwa wabunge labda wataalam kutoka katika sector mbali mbali. Kama ni mambo ya afya, kutakuwa na daktari pale.

**Com. Adagala:** sema hawataki, general kuwa waziri wa afya mnaelewa?

**Audience:** …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Mwishowe bunge ndiyo ita-recommend. The prime minister will make a choice halafu apeleke kwa bunge, bunge wajadiliane yote iko wazi hapa. Ikiwa mtu anataka ku-apply, ata-apply pia kwa Prime Minister lakini itakuwa Prime minister analeta proposals kwa bunge, bunge ijadiliane ndiyo huyu mtu anafaa education …(inaudible)… watu ishirini walikuwa proposed kwa kuwe minister of education wata-short list halafu walete mbele ya bunge, bunge ita-determine how many halafu ijadiliane kila mtu bunge ikikubali halafu prime minister, presidential assent.

**Interjection:** Can't they just say the nominated…

**Watako:** Tafadhali ngoja tumalize halafu utapewa fursa ya kuuliza maswali. Pia tunasema kwamba prime minister ndiye atakua mkuu wa serikali ndiye atakuwa juu ya hawa ma-ministers na ma-deputy ministers. Mishahara za hawa mawaziri na wasaidizi wao pia itatengenezwa ama itaangaliwa na salaries commission ama tume ya mishahara ambayo tume hiyo ndiyo itaangalia mishahara ya waalimu. Kutakuwa na makatibu wa wizara ambao tukonao hata wa leo na kila wizara itakuwa na katibu mmoja

kwa sasa itapata wizara moja iko na makatibu mbili ama tatu lakini kila wizara itakuwa na katibu moja. Halafau viapo vyote vya hawa mawaziri, rais viko nyuma ya katiba hii yetu. The first schedule za kabla ya kuingia afisini itabidi wape hizo viapo viko na maneno tofauti tofauti na mnaweza jisomea.

Katiba imepatia mamlaka hao wote, rais, mawaziri, waziri mkuu wote watashika mamlaka kwa niaba ya watu wa Kenya ambao wao ndiyo wako na mamlaka itabidi washike haya mamlaka. Hayo ya mawaziri, waziri msaidizi yatatekelezwa kwa wajibu itakuwa yanatakelezwa kuzingatia matakwa ya wananchi wa Kenya. Hiki ndicho kifungu ambacho kinatamatisha sehemu ya executive.

**Com. Adagala:** Haya ni maoni tulipata kutoka kwa wananchi …(inaudible)… ya prime minister. Prime miniser has to do …(inaudible)… executive rais with vice president and I got a proposal of the deputy prime minister where cabinet should come from. Now, ukianagalia hivi vizuri mnaona president ana kazi nyingi isipokuwa vile tulimwambia kulikuwa na fumbo sasa unafunguliwa laizma uende kwa watu tofauti tofauti wa ofisi zingine. Na kwa Act yet tuliambiwa devolve power sasa mtu ambaye alikuwa na swali kuhusu hivyo angezungumzia kwa bunge. Kwa sababu wabunge ndiyo walitengeneza hii. Devolve power kwa sababu wanajua shida gani hii ofisi iko nayo so kwa sisi tuliambiwa mkienda, hivi tukalima tukienda hivyo. Sasa mtu hawezi kuja kusema msingelima au mngelima mkienda huku.

**Interjection:** Swali yangu …(inaudible).. ni ya kwamba kutoa ministers wote kutoka nje sioni kama ni jambo nzuri.

**Com. Adagala:** Ukiteuliwa kuwa waziri utaacha hiyo kiti yako ya MP. Okay, it is a very simple story. Halafu unaenda kazini, minister ni kazi.

**Shem Oriedo:** Jina Shem Oriedo Livisa. Nauliza vile tuko na deputy minister incase minister amekuwa mgonjwa ama amepata mambo mengine huyu deputy atapata acting allowance au hii allowance? Two mahitaji ya kuwa president anatakiwa awe ameowa au amekuwa bachelor?

**Com. Adagala:** Hayo maoni yalikuwa mengi, ya wananchi lakini tukafikia kwa wakristo, alikuwa anafaa awe na mke mmoja, na waislamu wanasema ala na sisi na vitu vingine vyote halafu tukaona pengine iko punity kwa sititing president. Hata Kenyatta hatujui alikuwa ameoa au la au alikuwa na wanawake wangapi. May be that is what made people think this but we decided that we shall not put it for member of parliament even for councillors we shall not put it can be something that can be brought about but whatever you pass for the president has to apply to MP and councillor. Okay, you really have to think about it is not just punitive kwa sababu huyu hakuwa hivi au hakuwa vile lakini tutasema hiyo imefufuliwa tena okay.

**Ben Chumangi:** Majina ni Ben Chumangi. Proposal yangu ni mahali ya qualification za president. Mahali ya kwanza imeonekana awe mzaliwa wa Kenya citizen of Kenya mimi naona ingelikuwa bora awe mzaliwa halisi wa Kenya yaani *kindu kirnyanza* isiwe awe mhindi au hawa watatoka hapa Uganda azaliwe hapa halafu awe president. He should be a citizen.

**Com. Adagala:** Ujue sasa kuna familia moja which has two presidential candidates one in Ugana one in Kenya na ni wazaliwa.

Okay, Moodi Awori the brother is a presidential candidate in Uganda and he is presidential candidate. Na hata hivyo ndiyo wanasema hiyo pengine ulizuiliwa yeye kufanywa minister kwa sababu, the brother was in the other government. Haya mzaliwa wa Kenya halisi unajua mzee ako wapi? Ako hapa unajua you can even say how many generations, ni ngapi ndiyo mtu awe kwa sababu wahindi ambao wamezaliwa hapa ni wahalisi ni vigumu sana kuambia mhindi ambaye amekuwa hapa three generations yeye ni indigenous na wanapigania sana kwa hiyo you think about it some more utawapa hawa wajumbe wenu.

**Bulira:** Avedi Bulira tena nimeona hapa the same president awe mtu wa high moral intergrity na impeccable character itakuwa vigumu kupima hivi vitu vyote. Awe na high moral intergrity and impeccable character nani atapiwa itakuwa vigumu hilo ndio mimi ningependa nipendekeze tuseme awe mtu ambaye anaenda kwa kanisa ambalo linajulikana ama kwa msikiti.

Ya pili, nimeona pahali tumeambiwa au tumesoma pahali ati bunge itakuwa ikitengeneza timetable yao na tena hapa naona president anatakikaka a-dissolve bunge wakati fulani. pendekezo langu lingekuwa ikiwa kuna haja ya bunge kuwa dissolved awe ni prime minister ndiyo angefanya hivyo lakini asiwe president.

**Com. Adagala:** Kuna code of ethics and intergrity. Na pia kanisa tunaheshimu lakini wafisadi wengi wako kwa kanisa wanatoa fungo la kumi na watu wa kanisa wanakubali. Unajua hivyo inaweza tu kujificha kwa kanisa halafu niseme okay, lakini sipingi tutaongeza hivyo. sasa hiyo sasa tuone kama unaweza kurgezeka kwa sababu watu wengine wanapima word by the church okay. Halafu ya pili, someone pointed out that, normally I think it earned over from the other constitution but we could point it out, someone pointed it out to us I think it was a journalist unajua ilikuwa nyingi pengine hiyo ilivuka kama uchafu kutoka kwa hiyo constitution ingine. Hayo wacha tupeleke mbele ya tume ni kifungo gani? 142 okay.

**Iveda Rebecca:** Majina ni Iveda Rebecca. Pendekezo langu ni kuhusu this appointment of ministers. Ikiwa commissioners imetuambia hawa ministers itakuwa technically qualified na ikiwa some areas watakosa technical expertise, itakuwaje? Sasa itakuwa wale area watakosa ku-share power.

**Com. Adagala:** Not share power, you are talking about a minister. It is related you can be a land economist or you can be a land lawyer. Nafikiri tumeona Kenya imekoma tumeendelea na expertise nyingi sasa tunaona hatutakosa lakini can also be whoever is related to us lakini tukiwe hiyo, hiyo ndiyo italeta but is is related to find somebody. Lakini itakuwa serach. To run a ministry is not mambo rahisi na itakuwa search kabisa watu wapatikane ambao wataendelea. Kitu kimoja kingine nilifikiri mwanamke mwenzangu atasema kwa cabinet iwe affirmative action lakini ameacha. Mimi siwezi ku-propose na nafikiri haijakuwa although it says all officers but this is an important one also it is upto you if you want to do it or not. Ilisemekana kwa nini rais apiganie kura hizi zote azunguke nchi nzima ville mnaona inaendelea halafu hatakuwa na hizo nguvu zote. Tuliuliza hiyo swali watu walikuwa wanatuambia public spirited people will become president power baron. People who are looking for power this is not the position for them but it will be people who want to serve. People who are interested in serving the public and serving Kenya and improving Kenya. Si hivyo ndiyo ni kama umegeuka kabisa umekuwa sasa public serving unataka kufanyia Kenya sasa unaweza kupata two terms. Haya tunapita hiyo cabinet.

**Rhoda:** jina langu ni rhoda…. Mimi nauliza in Kenya hatujakuwa …

**Interjection:**…(inaudible)…

**Rhoda:** President anafanya kazi gani na vice anafanya kazi gani na waziri mkuu anafanya kazi gani katika Kenya?

**Interjection:** ….(inaudible)…

**Rhoda:***Kikila kundu kikupa na waziri mkuu dape ku ndakugenya waziri mkuu anyala kukula kii na vice na kole kii na president na kazi kii*

**Com. Adagala:** *Zingila.* Waziri mkuu wa Kenya alikuwa anaitwa Jomo Kenyatta *Olilanga*, halafu akachukua, wakasema waafrika wanafaa wawe na viongozi ambao wanafaa waone kabisa, wakachukua nguvu za governor akaweka, akachukuwa za prime minister akaweka, akachukua zingine akajiongezea za chairman ilikuwa president wa party akaweka akachukua zingine za bunge akakata ajakiwekea kama hii ya kuteuwa watu ok, ndio tunasma kiti cha waziri sasa kiko na vichwa vitano ni kama umezaa mtoto na vichwa vitano itakuwaje? Sasa ni vile tumefanya ni tunajaribu kurekebisha hiyo, tume ya kurekebsiha katiba. Hiyo ndiyo sababu yake moja hiyo powers za president zilichukuliwa zilinyakuliwa, wacha nitumie lugha ya Kenyatta mwenyewe, alinyakuwa alisema tulinyakuwa uhuru na sasa mimi nasema alinyakuwa nguvu hata za wananchi akajiwekea na imekaa hivyo tumeona haendi vizuri *kutimuli…(inaudible)…* lakini prime minister wa kwanza alikuwa Jomo Kenyatta

**Oyodi Rebecca:** Kwa majina ni Oyodi Rebecca, pendekezo langu ni kati ya 15 ministers hao, mimi napendekeza 1/3 should be women, na pia hata Prime minister napendekeza ikiwa president atakuwa mwanaume, mwanamke awe prime minister.

**Com. Adagala:** Hiyo ya president, ni vice president na deputy president, hiyo ni laini moja sasa umechanganya ndizi na viazi na maharagwe lakini ni chakula kizuri. Hii ya prime minister ingesema kuhusu deputy, watu wanasema hiyo ya president mmoja akiwa mume mwingine awe mke, mwingine akiwa mke hiyo ya vice president sasa Ngilu anasema atakakuwa president awe na vice wake mume, vice wake, na Kibaki akisimama awe na vice wake mwanamke. Lakini huwezi kuchanganya prime minister na president lakini unaweza kusema kwa hiyo kwa sababu nina vitatu moja awe mwanamke deputy, deputy na prime minister lakini si mimi kusema mimi ni kueleza. Siwezi kusema shika tu …(inaudible).. fikiria simama.

**Nathan Lughalia:** Mimi ni Nathan Lughalia. Mimi napendekeza mabalozi, high commissioners, ambassadors wawe wanateuliwa na bunge.

**Com. Adagala:** Ubaya unafikiria dictatorship ya president lakini watu hawajafikiria dictatorship ya bunge. Bunge limepewa vitu vingi sana, siku ingine itakuweko pengine itapunguzwa tena. Bunge ni nguvu sana na inaweza ku-dictate.

**Iveda Rebecca:** Majina ni Iveda Rebecca. Pendekezo langu kati ya watu watatu, president, vice na prime minister. Moja wao awe mwanamke.

**Interjection:** Prime minister atakuwaje?

**Iveda:** Kati ya watu wawili president na deputy wake akiwa president atakuwa mwanaume, mwanamke awe vice, ikiwa mwanaume au mwanamke atakuwa president prime minister …

**Interjection:** …(inaudible)…

**Iveda:** Ikiwa mwanaume atakuwa president, vice wake wawe mwanamke, ikiwa mwanaume atakuwa prime minister, mwanamke awe deputy prime moja.

**Com. Adagala:** *apakali bunyi mupola apakali pape ho dape nzia kuikala yakhapere. Pakhali pahapeda* there is no dunia. Tumemaliza tuendelee.

**Edward Ohare:** Jina langu ni Edward Ohare. Mimi ningependa kupeana pendekezo kwa u-president sijui kama hili jambo liliangaliwa. Mimi ningependa kupendekeza ya kwamba u-presidency iwe rotational kwa provinces kwa sababu itapatikana kwamba wakati fulani itakuwa watu fulani tu ndio kila mara wanachaguliwa kuwa president iwe kwa katiba ya kwamba hii presidency ilikuwa presidency province ingine sasa ipate nafasi otherwise provinces zingine hazitapata nafasi. Thank you.

**Com. Adagala:** Asante kwa kufufua hilo jambo la mzee kwa sababu lilikuwa kwa majadiliano mengi na tutasema limekuja tena. Hiyo ndiyo sababu tulifika hapa kuja tena. Pendekezo lako litapelekwa mbali na iko kwa maoni ya watu wengi kwa data here yetu sasa isibabaike ni wewe peke yako. Haya tuendelee…

**Fanuel Kaiga:** Mimi langu Fanuel Kaiga ni juu ya bunge na pendekezo langu ni ya kuwa bunge likipitishwa sheria au kitu wasipeleke tena kwa president halafu kile kitu kinakaa kule president anakataa na bunge imepitishwa. Bunge ambalo kwa sasa hivi kwa hivyo …(inaudible)…

**Interjection:** …(inaudible)…

**Kaiga:** Mimi nasema bunge tuseme tu bunge ambalo litakuwa likipitisha tu kitu wasipeleke kwa president ndiyo kitu tena kifanye kazi. Maana wamechaguliwa wapitishe maneno.

**Com. Adagala:** Mnajua it is new wine into old skin or new wine into new skin isn't it? Mnaelewa hiyo ya kingereza. Si iko kwa bibilia? Sasa tuwe tunafikiria kuenda mbele kitu kinafaa tufanya ni checks and balances. Council itakuwa inaangalia bunge iko hapo imetoka district bunge litakuwa hata tulikuwa na cartoon zingine kwa gazeti sijui kama mlipata. Bunge linaangalia judiciary au audit na judiciary linaangalia hivyo sasa checks and balances sasa haiwezi kuwa bunge linapitisha tu na hakuna mtu mwingine anaangalia hiyo ndiyo inaitwa dictatorship ya bunge imara hawawezi kuwa hakuna mtu atapitisha kitu peke yake. Pengine ungesema national assembly ikipitisha jambo liende kwa district council au ni watu wamechaguliwa tofauti or kitu kingine lakini huwezi kusema bunge ipitishe tu. Hiyo ndiyo dictatorship tunataka kuotka kwa hiyo na pia tena pito kuna hiyo ya kukataa ile ya ku-assent kama Act yetu ilienda for president for assent na kukubali kuweka signature hii ya commission lakini ingepelekwa

sasa president ndiye atachaguliwa hili apitishe au la pengine hata hangepata lakini ilienda kwa assent.

Lazima watu wote washiriki kwa kitu kwa sababu bunge ikikubali na president akubali hajakubali kutakuwa na shida. Sasa president anaweza haya mambo siyajui na yeye ndiyo head of state hayo mambo siyajui lazima aweke signature. Lakini ina njia ambayo inaweza kufanyiwa ili asikatae sheria inatungwa ili asikatae kama wamepitisha wanapeleka tu ajue na aweke signature. Haya tuendelee.

**Watako:** Sura ya tisa ni kuhusu mahakama na mahakimu na judge. Kitu cha kwanza ni kwamba uwezo wa mahakama utatoka katika wananchi na ma-judge, mahakimu itabidi wafuate matakwa ya wananchi. Itabidi wakati ule kesi zinapopelekwa mahakamani itabidi ziharakishwe sio kesi inamaliza muda mrefu. Technicalities itabidi hawa mahakimu na ma-judge wafuate sheria inavyotaka sio mambo ya technicalities utapata wanayaangalia mambo ndogo ndogo hii katiba inakotaza. Katiba hii imekuja na taratibu za kitu mahakam kuna supreme court ambayo sasa itakuwa korti kuu zaidi. Saa hizi kwa katiba ya sasa mahakama ya rekodi mahakama ya pili lakini katiba hii imebuni mahakama ya supreme courty ambayo itasikiliza kesi hata baada ya kupita mahakama ya pili. Kutakuwa na mahakama ya supreme court, court of appeal na high court.

Supreme court itakuwa na judge mkuu ambaye ndiye atakuwa anasimamia korti hii na ma-judge wengine sita watakuwa na uwezo wa kusikiza kesi zinazotokana na uchaguzi wa urais.

**Com. Adagala:** Ninaelewa sana tutakuwa na korti ingine juu, High Court. Hii pia itakuwa majadiliano mengi, wengine pia wakasema tuwe na constitutional court huko wengine wakasema tusiwe na kitu huko lakini mwishowe tukafika na supreme court na tukapeane kazi fulani atasema zitakuwa na high court juu yake. Supreme court na mmesikia ma-judge wangapi? Ni ndogo sana hapa for kichwa..

**Watako:** Wanapotekeleza jukumu lao, itabidi wawe huru wawe independent from other organs of the government. Itabidi watekeleze jukumu lao wakiwa huru. Mahakama hii ya supreme court ndiyo itakayo supervise hizi korti za chini ndiyo itakayoangalia kwamba hizi korti za chini zinafuata sheria. Mbali na supreme court ama korti ya juu zaidi kunayo korti ya appeal. Korti ya appeal ama the court of appeal itakuwa na rais wa korti hiyo na ma-judge kumi.

**Com. Adagala:** Tena mumesikia, rais wa court. Hii jina rais Kenyatta hakutaka mtu mwingine aitwe rais akanyakuwa yote sasa hapo itakuwa president.

**Watako:** Kutakuwa na high courts ambazo ziko sasa nazo zitakuwa na principal judges ama judges wengine mkuu zaidi kuliko hawa ma-judge wengine wa high court. Lakini siyo judge mkuu atakuwa principal high court judge. Na pia ma-judge wasiopungua hamsini ambao watakuwa korti hili nao watakuwa katika sehemu tofauti za nchi.

High court utaenda ukienda Kakamega hapa na high court Bungoma, Nyeri hivyo. Sasa kutakuwa na ma-judge ambao hawatapungua hamsini ambao ndio watakaokaa katika high courts. Korti hii itasikiza refer ambazo zimetokea katika korti za chini na pia itakuwa na jukumu la kwanza kusikia maswala tofauti tofauti. Ma-judge hawa judge wa high court na ma-judge

hawa wengine watachaguliwa na rais lakini sio kama sasa uteuzi huu itabidi ukaguliwe na bunge. Bunge lazima liwapitishe na rais sio kama sasa rais ameteua yeyote ule na pia kunayo qualification ambazo sasa zimewekwa mtu ambaye atachaguliwa kama judge lazima awe amekuwa mwanasheria na ako na ile experience ya 15 years kama mwanasheria either advocate ama magistrate lakini katika jukumu kabla ya kuchukua jukumu la kuwa judge lazima utakuwa uko na experience ya 15 years.

Waalimu wa vyuo vikuu watakubaliwa kuwa ma-judge lakini pia lazima watimize haya masharti wawe wamefunza kwa muda mrefu na watu hawa lazima wawe watu wanoastahili kutoka jamii wawe persons of the high moral integrity.

**Com. Adagala:** Mmesikia pale amesema high moral intergrity na pia awe na experience ya miaka kumi na tano. Mtu ambaye anastahili. Kuna judges wengi ndiyo mnaona ma-judge wanatuambia mambo hata kwa, let us say godfather this is love of our society anyway. Unakua na godfather na yeye anampandisha mwishowe unaenda unapata there are judges from one country kind of that thing. Then a president changes and judges come from another section of a country na hivyo na inafaa iwe watu ambao wana hiyo qualification are important because kazi ya judges ni kazi ambayo hasa intellectua a lot of intellectual work to be able to judge na ndiyo wanaweka hiyo kiwango cha elimu na pia there shoud be practice. They should have practised as magistraes as what as teanchers at the university so that they know what it says. Siyo kuchukua tu na kuwekwa hapo au kuchukua hii na hii iwe chaguo ya mtu mmoja mnaelewa?

**Watako:** Ma-judge hawa lazima wawe, na shahada ya degree ya sheria. Halafu kuna pia mabadiliko, ma-judge hawa itabidi wastaafu baada ya miaka sitini na tano, lakini wanaweza hata kustaafu kwa hivi wanapofikisha miaka sitini. Ma-judge ambao ni wafisadi watachunguzwa na commission ama kamiti ya bunge ambayo ndiyo itakayo zikiza malalamiko ya wananchi ama malalamiko ya watu wale watu tofauit ndiyo hao watu waendelee kuwa ma-judges. Kwa sasa, according to the transition provisions, watu ambao ni ma-judge saa hizi wanaweza kustaafu kwa hiari ikiwa wamefikisha miaka sitini ama wanaweza kuchagua waendelee kuwa ma-majudge na wanapochagua kuendelea kuwa ma-judge ni lazima watachukunguzwa mienendo yao ya ufisadi, utachunguzwa na kama itapatikana ya kwamba hawa watu walikuwa wafisadi watatolewa ofisini. Labda hii ndiyo inaleta mambo mengi na pia kuna korti fulani pia imebuniwa katika katiba.

Katiba kwa mara ya kwanza inabuni Kadhi's court. Hapo awali korti hii ya waislamu ilikuwa inabuniwa na parliamentary legislation, halafu katiba hii pia imetoa mwongozo ambao ni wa qualification za watu ambao watachaguliwa kama kadhi watu hawa pia lazima wawe na expertise, shahada ya degree ya sheria ya kawaida na pia wahitimu katika sheria ya kiislamu wawe pia watu wenye wanastahawiki wasiwe watu wafisadi. Katiba hii pia inabuni kamati ya kuangalia sheria jinsi mahakama ina-apply sheria hii inaitwa Rules kamiti na hii kamati itakuwa inaongozwa na judge mkuu ma-judge wa court of appeal, kadhi, magistrates hawa huwa watajadili wa mahakama kuu. Hawa ndiyo watakao wanaweza badilisha katiba katika kotini na pia wanawezahitaji mahakami ziapply sheria vile wanavyoona.

Katiba inabuni judicial service commission ama tume ya mahakama. Hii tume ndio itakayowateuwa mahakimu na maafisa wa kotin wa chini kama makarani na wengine. Afisa ya mkuu wa sheria wabuniwe katika katiba lakini mamlaka ya mkuu wa sheria yamepunguzwa kunaye director wa public prosecution sasa mtu huyu ndiye atasimamia mambo ya mashtaka katika mahakama

hapo awali mkuu washeria ndiye allikuwa mkuu wa mashtaka lakini sasa director wa public prosecution atakuwa huru kusimamia haya mambo ya mashtaka kotini. Pia, katiba imebuni mtu anayeitwa public defender, mtu ambaye ataona masilahi ya wale wasiyoweza kuajiri mawakili kuwasaidia katika kesi zao. Mtu huyu atakuwa anasikiliza malalamishi ya uma halafu ikiwezekana atakuwa anawapatia huduma za mawakili bila malipo.

Katiba hii inampatia rais mamlaka ya kusamehea wahalifu ambao wamepatikana na hatia kotini. Mawakili kitu cha mwisho sasa, wamepewa jukumu katika katiba tulipata malalamishi kwamba mawakili wamekuwa wafisadi sana lakini mambo haya yameangaliwa na katiba inasema kwamba mawakili itabidi wafuate sheria lazima wazingatie katiba hii na lazima watoe wailinde katiba hii. Pia kuhusu mawakili conduct ama tabia ya mawakili pia itachunguzwa na hii imedhibitishwa kwamba ufisadi na tabia zingine kama hizo hazitakubaliwa. Kwa ufupi, hayo ndiyo mapendekezo kuhusu mahakam na maafisa wa mahakama.

**Com. Adagala:** What about the district, what should it be, how should it decide which direction should people be going? You that kind of …(inaudible)… weka hapa African Traditional Court.

**Albert Kavechagi:** Naitwa Albert Kavechagi. Napendekeza kwamba hawa mahakimu wawe wakifanya kazi saa ishirini na nne sababu tumekuwa na cases nyingi na watu wamekuwa wakiumia katika hizi cells. Kwa hivyo napendekeza kwamba masaa ishirini na nne wawe wakifanya kazi.

**Nathan Lugalia:** Jina ni Nathan Lugalia, kwa haya maneno ya court sikusikia mkitaja court marshal na ikiwa iko …(inaudible)… anaweza kukaa kwa supreme court tena hii kesi ya mashamba hii iwe inasikizwa na wazee kuliko kupelekwa kortini.

**Com. Adagala:** Ukiwa na akili court martial ni ya military na hii ingine not land before kadhi inafikia high court, court of appeal kwa sababu waislamu wanasema unaenda unafika kwa chief kadhi halafu unakosa pale pa kuenda court of appeal na yako atakuwa anafika lakini pia hao wengine wanafaa wajue sheria ya waislamu …(inaudible)…

**Sabina Koki:** Mimi naitwa Sabina Koki Mulei. Maoni yangu kwa kitu ya katiba na wananchi sisi akina mama kama mimi, pendekezo vile mimi kama mjane kama tunatuma huko barua wasikii malilio yetu.

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Koki:** kitambo

**Com. Adagala:** Kuna social welfare hiyo, right, okay lilikuweko hapa tulitoa mwanzo miezi iliyopita. Haya basi tuendelee pengine haelewi. Devolution of powers hatuna hata wakati saa hii. Hii devolution of power ndiyo ilikuwa objective ya review moja na ingelikuwa mandate yetu moja sasa mtu kuleta swali kwa nini walizungumzia devolution of power hasa member of parliament anafaa aulize parliament. These are orders we were given from parliament sasa wangetaka isiwe hivyo ingekuwa parliament na devolution of power ni kitu very easy na wacha nimwambie power iko lakini vile iko, iko cut na kuna njia tatu ni

decentralization hii ambayo serikali inasema we are bringing the government closer to you kama district hivi. Lingine ni deconcentration pia inafanana sana na decentralization lakini deconcentration ni tofauti sana kwa sababu ni kuleta hiyo power na kuweka kwa wananchi ili wananchi washiriki ssa hata hiyo majimbo ni kweli ni majimbo lakini pia ni shirikisho hiyo ya kushirikisha wananchi pia wananchi wafaidike na pia wananchi wawe ndiyo wanatoa uamuzi. Mnalewa hiyo ndiyo devolution huwezi kuleta chini bila kuingia kwa wananchi lazima uingie kwa wananchi kwa kila kijiji kwa kila nyumba ndiyo iwe na maana.

Haya, devolution of power kuna principles nyingi za devolution of power. Kujitegemea self governance na remember sasa we are talking about the unity the district na chini na wengine tulitaka iwe province na chini lakini ikatokea district, endelea. National uity you have to work to strengthen national unity hiyo ya democrasia na wajibu accountable ya kutumia hiyo nguvu kwa accountability.

Economic development; kila mahali Kenya equitable checks and balances hii council ndiyo itakuwa chekcs and balances hata kwa district itakuwa ma-check na ku-balance wabunge wa assembly. Yes hiyo ya national and local resources kama mashule, mahospitali, bill za dawa, hiyo nyuma tumesema hizo za ministers hiyo yote. Hiyo ya kutao nguvu zote kwa central governmet decentralize so that it comes down. Na hiyo ya kuleta kwa watu huduma ya vitu vya muhimu, essential services effectively and economically. You know very well the council doesn’t do this very well, the council has no way, it doesn’t happen for them very well, because they don’t have the national resources to use all the local resources. *Mumanya mtula* sa councillors lakini wamefungua sasa hii ndiyo itawafungua ili wawe wanatekeleza hiyo mambo. Na councillors tuliona ni watu wanataka kufanya kazi wamechaguliwa sasa wawe na hiyo nguvu kusaidia wale wachache kama minorities …(inaudible)… okay hiyo pua ya kushiriki mashinani na pia juu.

**Watako:** Katiba hii sasa ina mfumo. Imeweka mfumo wa kijiji, serikali ya kijiji. Serikali ya kijiji itakuwa chini ya watu sita ambao watachaguliwa na wana kijiji wenyewe. Hawa ndiyo watakaoendesha maswala ya kijiji pia kutakuwa na serikali katika location. Location hii kwa sasa kuna chief lakini, kutakuwa na serikali ya watu watatu ambao watateuliwa kutoka kwa vijiji moja wao atakuwa ni mama ambao wao ndiyo watatawala ama watashikilia maswala ya location nzima halafu pia kutakuwa na serikali ya wilaya. Serikali ya wilaya itakuwa na wanachama wasiozidi thelathini ambao pia watachaguliwa na wananchi kutoka kwa location na pia watakuwa na mkuu wao ambaye ataitwa administrator. Serikali hizi zitakuwa na uwezo wa kupitisha sheria fulani. Hapo awali tumesema kwamba ni bunge peke yake ambalo liko na uwezo wa kupitisha sheria lakini pia serikali hizi ndogo ndogo pia zitapewa uwezo wa kupitisha sheria ndogo, sheria zinazohusu maswala ya ushuru, maswala ya huduma labda kutupa uchafu na pia maswala mengine halafu serikali, central government pia itawajibika kuwasaidia serikali ndogo ndogo hizi na maafisa. Ama, pia hizi serikali ndogo ndogo zitakuwa pia na uwezo wa kuajiri maafisa wao wenyewe ili kuona kwamba shughuli za serikali hii zinaendeshwa kawaida.

Na katika hali ya kuona kwamba resources ambazo ziko katika sehemu za mashinani zinatumuka ama zinanufaisha wale wananchi serikali hii itakuwa na uwezo wa ku-manage hizo resources zenye ziko mashinani kama mko na mawe ama madini ni serikali hii pia itakuwa na uwezo pia kuona kwamba national government na local ama devolve authority zinapata ama

zinanufaika na hizi resources. Ratio yenye itakuwa ama ile hali ya uhusiano ambayo itakuwa kati ya serikali kuu na hizi serikali pia imeandikwa katika  katiba kuhusu utuezi wa maafisa wenyeji kama kwa katiba ya sasa serikali kuu ilikuwa na uwezo zaidi wa kuvunja hizi serikali za wilaya lakini kwa sasa hizi serikali za wilaya zimepewa uhuru haziwezi vunjwa na serikali kuu kiholelaholela. Hizi serikali za district councils zitawajibika ziwe na uhusiano mzuri ama uhusiano wema kati yao. Tuseme ikiwa watu wa Vihiga ama council ya Vihiga inahitajika iwe na uhusiano mzuri na council ya Kakamega ili kuwanufaisha watu wanaokaa katika sehemu hizi. Halafu mwisho tunayo sub-location. Eneo la sub-location ndiyo sasa itakuwa kijiji. Halafu kijiji kitakuwa village tunavyoelewa, lakini itakuwa sub-loation, maana ya council hiyo mnajua itakuwa sasa village council, location and district council.

**Com. Adagala:** Hilo lilikuwa swali muhimu sana nchi nzima, wengine hawakuta majimbo vile walikuwa wanaita lakini ukizungumzia nao sawa wanazungumza our roads, barabara zetu hazitengenezwi hawa councillors sasa mwishowe wakisema hivyo wanasema kama huko Kiambu wanasema sisi ndiyo tunauza kahawa na look at our roads. Which means they want to benefit from the money which comes from kahawa which means devolving power they want to have a say in it. So, are there any questions, there or we continue. We can continue.

**Interjection:** Level of education.

**Com. Adagala:** Ya nini?

**Interjection:** Village elders, district

**Com. Adagala:** …(inaudible)… I think we discussed it I don’t know if it is here.

**Bulira:** Mimi napendekeza ya kwamba kama village councills wale ambao watakuwa members wawe na elimu ya standard seven and above. Locational wawe juu ya standard seven form two and above. But below form four, district the councils.

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Bulira:** District governance wawe wale ambao wako na kiwango cha elimu ya form 4, provincial councils 4 and above.

**Com. Adagala:** Okay hiyo ni proposal tuendelee. unajua sehemu zingine za nchi hii kama tulikuwa huko Laikipia na wakasema in the whole district they have about six graduates. So, I said my God that is how many graduates are there in my family. You see that so some people really have a difficulty with this one sometimes it might change from place place haya tuendelee, mmeelewa devolution. Tumefanya rahisi sana nafikiri mtasoma tu na kuelewa nafikiri mlikuwa mmekubali sasa hatuna shida sana hapo lakini mjue ili watu wanaenda kwa national constitutional conference hili litakuwa jambo kali sana so just don’t sit and think nobody you have to defend it even have you have to defend it.

**Watako:** Sasa tuko kwa sura ya kumi na moja ambayo inahusu shamba na mali. Katika mswada huu tunayo mapendekezo ambayo ni ya muhimu ambayo yanafuata hivi lazima kuwe na usawa katika kupata shamba equitable access to land ule usawa.

Katiba hii inapeana umilikaji wa shamba katika mara tatu. Shamba itakuwa ya mtu binafsi ya familia ama ya jamii, community na ya uma. Na shamba hii itakuwa classified according to the geographical region halafu mtu asiye raia wa Kenya hatakuwa na uwezo wa kumiliki ardhi chini lakini atakuwa na uwezo wa kukodesha ardhi atakuwa anaweza ku-lease lakini hatakuwa na uwezo wa kumiliki ardhi kabisa.

**Com. Adagala:** Hili, kuna watu ambao walipewa 1999 lease some of them are not even Kenyans. Wazungu na huko Laikipia tuliambiwa kuna 800,000 acres being run by political white people 24.

**Watako:** Serikali pia imepewa uwezo wa kumiliki au kutoa ardhi ya watu binafsi kama inahitajika na matakwa ya uma ama ni the public interest la sivyo serikali haitakuwa na uwezo wa kumiliki kwa nguvu kunyang'anya mtu kwa nguvu ardhi yake. Tume ya shamba ambayo itachunguza mambo ya shamba sasa imebuniwa chini ya katiba haitakuwa ya muda kama ilivyo sasa itakuwa permanent ambayo itakuwa inachunguza mambo ya shamba, mambo ya umilikaji, titles na vitu kama hivyo.

Halafu kupata cheti cha shamba itarahisisha kama saa hii kuna process ndefu, hizo process za kupata title ama shamba zipunguzwe. Mwisho kuna interpretation lakini hiyo sio kama ni muhimu kwa sasa.

**Com. Adagala:** …(inaudible)…

**Watako:** pia

**Ivedi Rebecca:** Kwa majina ni Ivedi Rebecca. Swali langu, ni kuhusu mashamba. What will the title deed read, will it include a woman or it would just be for a man?

**Com. Adagala:** Why are you asking such a question? Ownership, many communities first of all Maasai women say they want land owned first of all by the whole community, because men have sold the land. Half the land is in Kikuyu hands. Many of them were selling them in bars for something very small and such kind of things so wao waliuliza first of all iwe community land, secondly wafanyiwe a title deed itengenezwe ili majina ya mama na baba na watoto au wamama kwa sababu inaweza kuwa zaidi ya mmoja wawepo kwa sababu shamba isiende hiyo. Haya wengine walisema pia hayo lakini ilikuwa kwa sababu tofauti. Ni kwa vile mtu akiaga dunia sasa mjane anahangaika amam aliuliza hapa mambo ya wajane, wajane wanahangaika hapo pia ikasemekana iwe joint registration.

Jambo la tatu ni hilo urithi wa wabibi wamezaliwa hiyo nafikiria iko kwa succession wana haki ya kurithi. Sasa hiyo ndiyo itakuweko. Lakini akina mama unapelekea kitu hapo kwa sababu wamama wanataka registration lakini ni urithi wa vijana so its important hata hiyo itakuwa urithi wa msichana baadaye itabadilisha vitu vingi lakini …(inaudible)… viti vingine tuliwacha itakuwa tu not in the law not in paper lakini ziko hapa.

**Com. Adagala:** …(inaudible)… Hii habari ya mashamba, mimi naonelea watu wengi wasiwe na acre elfu tatu mia nane, elfu moja na sisi hapa kuna watu na nusu acre, acre moja. Kwa hivyo mimi naonelea maana shamba inatuluezo watu wa Kenya na

watu wengine wame-fence mashamba yao hayatumiki na wengine wanapata tabu. Kwa hivyo kuwe na sheria mtu asipite acre fulani.

**Com. Adagala:** Kuna mambo mengi ya mashamba. Ya kwanza wanasema there is no idle land kwa sababu ndiyo unachukuliwa kuna land haina watu. Pili, wamesema Mungu amepeana shamba kwa kila mtu kila kabila ina shamba yake, wake ndio hao unaona si hao makaburu au matajiri wame-fence lakini lengo lenu ya kupata kule kwengine sema Aids imezidi mwanadamu anaoa mwanamke kutoka Luoland sijui kwa nini wanasema Luoland halafu yeye anakuja na ndugu za huyu mme wanafuata na wananunua nafikiri wana … they are feeling helpless lakini hapa nikiketi hapa na Prof. Salim na Phoebe Asiyo watu wa hapa walisema wanataka industrialization yaani hii ni city iendelee kukua city hakuna haja unajua sasa hii katiba tumetengeneza ambapo Kenya wanategemea shamba na mtu aambiwe watu rudi mashambani na chukueni hii mununue ikawa hiyo pre-occupation lakini unaweza kuwa tu na mahali unaishi na unafanya kazi na huna haja ya shamba lakini hapa watu walisema industrialization kwa hii pendekezo zenu za shida. Pengine hiyo ni mapendekezo ya watu ule

**Interjection:** Sikusema hivyo, mimi nilizungumzia mambo ya mashamba

**Com. Adagala:** Ilikuwa iko kwa ripoti kuna watu walisema mashamba nakuambia, hakuna mashamba kama hayo, watu wa Lugari wamesema wacha nikuambie ili tusi… wamesema tulihama tukitoka Maragoli na Bunyore tulikuja *ilikhusia* acre mbili kununua acre kumi nimekuja nimegawanyia watoto wangu waliobaki wamerudi kwa acre mbili na wako kwa acre mbili bila ya maendeleo ya Vihiga. So, it's a complicated thing, but tunasema nilikuwa najulisha ile ilisemekana hapa hata *shiwatsuri* nawe mnaona hii ni kama gold na pia gold iko hapa watu wakisema madini yako hapa lakini sina haja tuzungumzie natural resources tukienda lakini hayo maoni iko hapa.

**Caleb Juma:** Nilikuwa napendekeza mimi Caleb Juma, kwamba wale watu tuko wasio na zaidi ya acre…

**Com. Adagala:** Hiyo ni kama primary level ya, he was giving views, you were here haya, pia hiyo inakwenda mbele ya sheria yameshikana watu wamenyakua mashamba hayo pia yatakuwa part of ufisadi. Okay, wale wamekata misitu hata Watiriki wamesema Maragoli wanakuja hapa wanakata misitu halafu wanaita vururu wanakasirishwa na jina hiyo lakini wanakata misitu yao loose, sasa watu walienda Tiriki tulikuwa na wewe, wanataka misitu yao iwe thabiti. So ni vile nimeambia watu wengi what we have is a peasant constitution on the land. Unaongeza watu kama ndio mlikuja kutoa maoni nao watu wa juu juu walifikiria hawana haja sasa hata hiyo mashamba yao itachunguzwa. Wacha tuache hivyo mtasoma zaidi kama tumeripoti tofauti mtatuambia.

Kuna jambo lingine kuhusu shamba unajua lazima sehemu za nchi hii ziwe towns kama Kawangware. Kawangware ilikuwa na mashamba ya the independent times na mahindi ndani, na Kangemi, sasa hao watu ni matajiri kwa sababu hao watu wametengeneza tu vitu vidogo vidogo. Haya kuhusu devolution pia inafaa mjue kazi nyingi zitakuwa located in the district. Hatujasema hivyo, lakini tutakuwa kwa district tuna-devolve powers, tuna-devolve employmet to the distrcit mjue hivyo ili mjue district itakuwa ni muhimu sana. Haya land and property ndio twaita environment kwa …(inaudible)…

**Albert Kavehangi:** Naitwa Albert Kavehangi. Kuhusu mashamba ningependekeza kwamba mashamba ambayo yanakaa bure ni lazima yafanyiwe mambo fulani yasiwe bure. Lazima yalindwe na sikuona pale tumetaja katika hii katiba.

**Com. Adagala:** Lakini wananchi wamesema mtu awe taxed au apeane shamba igawiwe watu wanaosema kutumia na pia hii kitu ya one job one person inaingia kwa hivyo mashamba. Mtu ambaye ana mashamba ya acre hamsini mjini Kitale na ako officer Nairobi achague atalima au ataenda kwa ofisi. Hiyo ndiyo one person, one job?

**Watako:** Ya pili, mazingira na mali ya asili ambayo ni sura ya kumi na mbili. Kwa mukhtasari tu sura hii inasema kwamba katiba imelinda mali ya asili na mazingira na kila mwananchi amepewa uwezo wa kupeleka serikali mahakamani ikiwa inakiuka huu utaratibu lazima msitu, udongo na vitu kama hivyo vilindwe na katiba. Mali, msitu ya uma lazima pia ilindwe na katiba. Bunge imepewa uwezo wa kutoa sheria au kutunga sheria kuhusu utunzi wa mali ya asili na mazingara. Mazingara na mali ya asili lazima yatunzwe kuwanufaisha watu wanaoishi katika sehemu ambazo mali ya asili au mazingara yale yanapatikana. Kwa mukhtasari tu hivi ndivyo sura ya kumi na mbili inatueleza.

**Com. Adagala:** …(inaudible)… mazingara, equitable development kama hapa nimesema kuna madini mengi na rivers hata zinakauka na vitu vingi …(inaudible)…. International treaties inafaa zi-comply na environment lakini mnajua treaty mbaya moja sana ya Egypt ile ya 1928, tulizungumzia ile inasema Nile waters ya hiyo pengine haikutajwa hivyo lakini district kutoka Marakwet hata watu wa Marakwet walisema rain is a natural resource. Kutoka huko mpaka Rarieda, Bondo hizo zote zinafaa kuingia hizo zote zinafaa *zishiriala* tukiambia watu wa Egypt lazima watu watoe kitu hawawezi kuwa na hiyo faida ya kupata maji kwa sababu hiyo ni natural resources.

**Com. Adagala:** Public finance

**Watako:** Nilikuwa nimechoka lakini tutaangalia sura ya kumi na nne, ya kumi na tatu ambayo inagusia mambo ya pesa za uma na uhaki, accountability kwa fedha za uma. Kwanza, sura hii ina-legalize ama inatakataza ufisadi. Katika juhudi hizo za kutuhimiza ufisadi, ime-establish afisi under the auditor general ama mkaguzi wa vitabu za serikali na ofisi ya controller general ambapo kwa katiba ya sasa alikuwa afisi moja na mtu moja lakini sasa hadi ofisi mbili tofauti na iko na wajibu tofauti.

Serikali sasa inawajibika kutumia pesa kuwanufaisha watu wa serikali, kuwanufaisha uma. Juhudi hizi zitaangaliwa na bunge. Bunge limepewa kipawa mbele katika ile haki ya kuendesha mali ya uma. Budget na matarajio ya pesa zingine za serikali zitahidhinishwa na bunge pia kuna zile contigenices ama pesa ndogo ndogo ambazo huwa zinahitajika kutoka kwa kiti ya uma lazima itakuwa authorised na parliament. Hakutakuwa na ile kutoa pesa kwa pesa za uma ama kwa consolidated fund bila approval ya parliament. So kwa mukhtasair ndio sura hii inaoengea.

**Com. Adagala:** …(inaudible)…utufi

**Watako:** Tutaangalia pia kwa mukhtasari sura hii ya ni juu ya utumishi wa uma kwa sura hii. Kwanza watumishi wa uma watakuwa watu ambao wanatoshea kushiriki, mamlaka ambayo wamepewa na watakuwa watu ambao sio wafisadi.

Watachunguzwa mienendo yao na pia wako maafisa wakuu wa serikali itabidi watambue mali yao na jinsi walivyopata ile mali kabla ya kushirikia wadhifa katika vyeo mbali mbali. Katika sura hii pia kuna kikosi cha polisi ambacho hapa awali kilikuwa kinaitwa police service police post sasa kitakuwa kinaitwa police service. Hii ni katika juhudi za kufanya maafisa wa poilsi wahudumie uma na sio kuwanyanyasa watu. Sasa watakuwa watumishi wa watu. Pia kuna correctional services.

**Com. Adagala:** Huo upande mwingine, walikuwa wakisema traffic police wachague kama wachukue mishahara yao kwa roadblock au tuwalipe. Sasa ime … sasa ilikuwa polisi na provincial administration na judiciary, hao ndio walikuwa wanalinda uma sana ndio tumetaka ndio iwe services sio force, iwe police services. Na tumekuwa na national one na pia tumekuwa na hiyo ya district watu walisema kujua hao polisi ni akina nani, hatutaki watu wa mbali kuja kuwanyanyasa wajue huyu mtu apate recommendation kutoka kwa chief apate recommendation pia kutoka kwa shule na awe mtu wa hapo tumjuse ili ufisadi upungue. Pia badala ya prisons ama idara ya jela, kunayo correction services ambayo ni idara ya kugeuza tabia za watu. Hii ilikuwa juhudi ya kuona kwamba ambao wamehukumiwa na mahakama wanafaa tabia yao inabadilishwa sio kama sasa mtu akishikwa mtu anapelekwa mahakamani na anarudi amekuwa sugu zaidi. Kwa mukhtasari hayo mapendekezo ya sura hii halafu kuna sura ya kumi na tano ambayo ni the defence and...

**Caleb Juma:** Mambo haya ya polisi, we have recruited from the locations kwa sababu wakipeleka kwa district watu watakuwa wanaletwa pale na kila location hata zingine hatuna watu kwa police force at locational level.

**Avedi Bulira:** Mimi nazungumzia, Avedi Bulira. Mimi nazungumzia mambo ya civil servants, wakati mwingine nilisimama hapa nikasema civil servants wawe wasijishughulishe na biashara, wafanye kazi moja huko na waache farmers washughulike na mashamba. Nilisema civil servants wanatumia mamlaka yao, simu za serikali kulima mashamba yao na wengine hawalimi. Nilisema civil servants ndiyo waliingiza magendo hapa kwa kuweta makoti kwa viti na kwenda nje ofise zinakaa bure, sioni ikitoea hapa.

**Com. Adagala:** Ngoja hatujamaliza Ndegwa, commission isn't it? Haya wacha tufike kwa hiyo ya public service …(inaudible)…

**Albert Kavechagi:** Jina tena ni Albert. Hapo kwa police service napendekeza kwamba wakati mwingine hao polisi wanatunyanyasa na ukiwa tuseme, hii Africa imetunyanyasa sasa ni pointless tena kuenda ku-complain kule mbona tungekuwa na pahala fulanni amabayo tungependekeza malalamiko yetu ili ikiwa mkuu wa police hapa anatunyanyasa tuwe na pahali fulani pa kumpeleka.

**Com. Adagala:** Protection ndiyo hiyo iko ndani okay. Tuendelee sijui tena

**Watako:** sasa tunaendelea na sura ya kumi na tano ambayo ni ulinzi. Sura hii iko juu ya ulinzi. Kwa mara ya kwanza vikosi tofauti za jeshi zimebuniwa katika sheria. Ingawaje rais bado ni amiri jeshi mkuu lakini pia katiba hii imebuni a security council ambayo itasaidia rais kama ni ku-declare vita ama ni kutangaza hali ya hatari. Decision hiyo itafikiwa baada ya mjadala wa

national security council ambayo iko na vice president, prime minister watu kama hao. Wakuu wa vikosi tofauti vya jeshi ndiyo watakayo amua ikiwa kutakuwa na hali ya hatari kama vita. Tunasema kwamba rais bado atakuwa amiri jeshi mkuu halafu decision aama uamuzi wake hataifikia yeye peke yake atafikia baada ya mkutano wa hawa watu wote.

Sura ya kumi na sita ni uongozi na usitahiki. Sura hii ilipendekeza kupigana na ufisadi. Kabla ya maafisa wakuu wa serikali nitarudi hapa tena kabla hawajachukua hatamu za uongozi itabidi watambue mali yao na jinsi ulivyopata pia kunayo imebuniwa hapa tume ya ethics and integrity. Tume hii ndiyo itakayochunguza mambo ya ufisadi hapo awali kulikuwa na tume lakini haikuwa ndani ya katiba lakini sasa katiba inabuni tume ambayo itakuwa inaangalia mambo ya ufisadi, itakuwa inapeleka watu wa ufisadi mahakamani na pia itakuwa imepitisha sheria za kupigana na hayo mambo ya ufisadi. Kwa mukhtasari hayo ndiyo mapendekezo ambayo yako katika sura hii ya kumi na sita. Hiyo mtasooma na mtaelewa.

**Com. Adagala:** Hapa na tume zingine ambazo, haya za tume hizi ni kutekeleza constitutionalism ku-institutionalize constitutionalism. Put it into institution so that itasaidia katiba kuendesha na parliament kuwe na uma ili mambo ya katiba idumu na isiwe tu kitu cha kurandaranda nafikiri mnaweza kujisomea hiyo, ni tume kumi hivi. Nafikiri ni rahisi kusoma hapo si ngumu sana lakini ni kumi halafu tukimaliza hayo mnaweza kusoma na muone ni nini mnaweza kuongeza. Kuna vitu kama tume ya vitu kama utamaduni, mtu alisema kitu kingine sijui ni nini hiyo, vingi vinaingia kwa human rights commission itakuwa kama watu watakimbilia huko halafu kutakuwa na kamati humo ndani.

Lakini, angalia uone kama kuna kitu ungependa kiwe kwa tume utaleta mbele mtawapa hawa wakilishi wenu waje nayo lakini kitu kitawafurahisha sana ni kusoma hizo tume na pia hawa watu na tume watakuwa watu wa high integrity. Kama una ufisadi maishani mwako itakuwa ngumu sana kupata kitu chochote cha uma here sababu utachunguzwa na kuonekana vile uko kila kitu kitakuwa wazi. Halafu kuna hizo transitional and consequential provisions ambazo tumesema hapa na pale lakini mzisome hizo ndizo zinasema hiyo daraja ya kuruka kwenda mbele kama hii katiba itakubaliwa na kitu rahisi tu hiyo ya kuanza ni kuhusu mipakka ya Kenya na ya pili inahusu kila schedule ina deal na issue fulani ambayo iko na details ingine mtaona ni numbers hapo lakini mtaeleza hizo ni mumbers hizi ni nini na uwezo wa kusoma halafu hata imewekwa district ni nini. Kama Western ni Malava, Lugari, Kakamega, Butere-Mumias, Vihiga, Mt. Elgon, Bungoma, Teso hiyo sasa iko kwa constitution hiyo ndiyo imefanya hizo district ziko kwa constitution hii na haziwezi kutolewa au mtu hawezi kwenda mahakamani kuzitoa ni constitution. Halafu tunamaliza na hizo zote ziko hapo hiyo ya mambo vitu vyote transitional natures ni zingine schedule.

Hapa mwisho ni commission na human rights ziko hapa, zinaelezwa hizo za clashes na watu ambao walifanyiwa bila ya kuuwawa na vingine. Human rights abuses zote ziko hapa. mtasoma. Haya keti tu hiyo yote tumemaliza. Kitu kimoja mtu aliuliza swali mbeleni kulikuwa na constitution ilikuwa imeandikwa hatukujibu kwa sababu hata kwa CCC, sio swali watu wengi waliandika constitution kama huyu Bulira vile anaonelea na wengine hapa unaweza kuandika constitution umalize iwe tu na guide na utaandika. Wakili aliandika, NGO's zingine ziliandika halafu tulikuwa na moja ambayo ilikuwa kama 'dummy' wacha nieleze wazi ilikuwa kama 'dummy' ili tujue inaweza kuaje na wengine wakachukua wakasema hii ndiyo constitution lakini haiengewezekana hatakuwa tunajadiliana mambo tulikuwa tumetoka tu hapa sivyo ndiyo wengine wakachukua ndiyo wakaenda

wakasema mbeleni hii nidyo imetolewa nidyo katiba na siyo kweli.

Kuna chapters lazima ziwe kwa constitution sasa hiyo ndiyo ilikuwa and hivi vyote kila laini hapa tulijadiliana kama tume na tukatoa. So, I don't know what else to say about that kwa sababu watu wa magazeti wakipata kitu kama hicho ni kitu inakuwa hii ndiyo kidamudamu. Kuwa kitu kingine kinaitwa reproficosity reciprocal hiyo ya ku-reciprocate unambia zawadi. Mimi mtu kupa zawadi tuna-reciprocate au …(inaudible)… kitu kama hicho. Mnabadilishana na hicho kitu kuko kuna sehemu moja na international treaties lakini nafikiri pengine mtu angefanya iwe kama kura citizenship wale watu ambao nchi yao tuna citizens hapa wawe pia wanatupa citizenship kwao hivyo. Kama India, watu wanafaa wawe wanaishi India wasiwe na hostility vile wako na watoto wetu wanasoma, huko na wapi Uingereza na wapi ingine.

Watu wengi wanatoka lakini namueleza tu, kitu kama hicho sijui France na reprocity kwa nini kuna kitu fulani lazima wawe pia uwarudishie kuna kitu hapa nakikumbuka sana lakini na pia unajua kwa nchi zingine watu wa nje hawawezi ku-own land kama Norway nilienda huko wakaniambai hata iwe na mali gani huwezi kununua ardhi yetu hata acre moja hata plot, so things like that probably the coutry we have we buy they should be bale to do that in other words so that they don't do it one way ubaya wa ukoloni iko one way na hiyo ndiyo ukoloni mambo leo. Haya kama mtu ana mambo ya ku-wind up aleta au kama jambo lingine limetokea.

**Avedi Bulira:** Mimi ni Avedi Bulira. Sina mengi ya kuongeza ila kutolea shukrani hii commission inafanya commendable work imefanya kazi nzuri kabisa. Tunatakikana wote tuwaunge mkono waendelee kumaliza hii constitution na iwe ikiletwa itumike wamefanya kazi nzuri asante kwa kazi hiyo nzuri.

**Com. Adagala:** Wale wakiwa mama

**Speaker:** Hata lenga tena ile kitu nilisahau kuuliza ni juu ya hizi land triburnals. Sijui kama zimetolewa ama?

**Interjection:** …(inaudible)… angalia huko ndani.

**Com. Adagala:** Ndiyo mjue haya ni maombni yenu sasa nitatoa wapi …(inaudible)…

**Nathan:** Mimi ni Nathan…(inaudible)… kitu kidogo tu kwa …(inaudible)… this process. Police services police anaweza kukushika huna makosa na anakuambia toa kitu kidogo usipotoa anakuwekea kitu fulani halafu anakupeleka kortini. Ningependekeza kwamba hawa polisi waondolewe ikiwa wanawakuta wako na hiyo ufisadi

**Com. Adagala:** …(inaudible)…. Hapa hakuna ufisadi …(inaudible)…

**Albert Kavehagi:** Basi yangu ni machache, ni kwamba ama ni kuwapongeza nyinyi na napendekeza kwamba vile tumepata maripoti kwamba mmepelekwa kotini napendekeza kwamba hayo mambo yatolewe kwa sababu …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Mzee nilisema hata ikiwa kortini hata Lumumba alisema kwa T.V, basi tutaenda lakini Hotel Intercontinental

ilituambia itatufanyia outside catering kwamba Nairobi ni kama watu wote wako upande wetu sikuona sababu ya kuwa upande wa ma-judges wafisadi sikuona mimi

**Shem Oriedo:** Mimi ni Shem Oriedo Luvisa. Napongeza kazi ya commission ambayo iliunda katiba nami nasema kwamba ma-judges au yeyote ambaye haungi mkono kazi ambayo walifanya washitaki sisi watu wa Vihiga ambao tulitoa maoni yetu. Thank you.

**Com. Adagala:** Wasiambie washitaki bunge sasa inasema mshtaki constituency forum.

**Audience:** Eh

**Com. Adagala:** Wamesema msisome hiyo mambo mlijua hivyo. walisema hii chapter isiwekwe hapa.

**Awisi Kwao:** Kwa majina mimi ni Awisi Kwao. Mimi naonelea hii commission ya katiba imefanya kazi nzuri lakini hii kazi yenu inatakikani tukienda kwa general election tutumie hii katiba mpya. Asante. Hii katiba mpya itumiwe kwa hii general election inakuja

**Rhoda:** Jina langu ni Rhoda Kavetsa. Mimi nafurahi kwa hii katiba ambayo inatengenezwa siku ya leo kwa maana katiba ya zamani ilikuwa inasahau wanawake na mimi naona siku hizi wanawake tuko mbele hata tuko ndani ya katiba iendelee namna hii na sisi tutapata hata wanawake wapate uminister wawe wakiongoza sisi.

**Tume:** Mimi kama representative wa disabled katiba constituency ya Vihiga ni jambo la kwanza ningepongeza madama Kavetsa na timu yake *indala* wamefikira wamefanya kazi mzuri, one, two sikuwa nikijua kwamba hii kazi itafika hapa mahali ilipofika na kama inafika then wamefanya jukumu la busara. Tatu itakuwa ni vizuri kwa hii katiba ya sasa naona kama kidogo wanajaribu ku-sense na kuelewa ya kwamba wananchi wasiojiweza na walemavu, ni walemavu tu miguu lakini kuna wengine akili zinafanya kazi ambao serikali ikiwahusisha kwa mipango yao tunaweza tukafanyae na ninafikiria madam Kavetsa na mara nyingi anavyozungumza ni kama anatuangalia walemavu anaona ni kidogo tumehusika na kwa sababu tumehusika na nikaandika memorandum kuna kitu kimoja tu sijui kilichukuliwa vipi sababu tulikwa tunaomba serikali katika budgeting yake iwahusishe walemavu ili wawe catered na serikali swala hilo ndilo sikulisikia lakini natarajia marekebisho yatafanywa. Asante.

**Com. Adagala:** Upendekezewe na ilikuwa unapendekeza asilimia kumi na tano ya jobs ziwe kwa walemavu kwa sababu wako asilimia kumi na tano. Katiba ilisema itatendeka katiba ikikosa kusema haitatendeka. Hata hiyo ya budget unasema pia itatendeka nidyo ilikuwa hiyo commission ya walemavu kuna bill ambayo ni ya walemavu inaenda mbele na mswada huo unasema iwe na commission sasa hatuwezi kuweka commission zote hapa lakini kwa human rights itakuwa committee ya walemavu. Sasa hiyo ndiyo vitu vinafaa tuzungumzie tuone itakuwa vipi lakini mki-push mkiwa organised kama wale wa South Nyanza ambao wamesema watasimama bungeni na councillor sasa pengine mnaweza kuwa na nguvu kwa sababu walikuwa wanasema na nguvu sana.

Walemavu wote duniani wameungwa nguvu sana sasa tuatendelea hivyo. na mila zetu mubadilishe musiseme tu serikali nyumbani mwenu kila mtu kwa jamii yake ana mlemavu ili nimeonga la kutokuwa na macho nimeanguka hata nimeshukuru Mungu ni miujiza ninaona kidogo.

**Mponga:** Mimi jina langu naitwa Mponga na mimi nashukuru sana kwa sababu vile mnasema nimeandika tu. Nyinyi mzidi kushitakiwa lakini mfikishe maneno, ule ambaye anaona chuki kwa maana mnafanya katiba huyo ni mchoyo hapana fanya kazi vizuri. Nyinyi …(inaudible)… mambo iendelee mbele kama kana sisi bado tuko hai tuone

**Com. Adagala:** Watu wa Kenya asilimia tisaini ni maskini na wanataka mabadiliko na mnajua wacha niwaambie sote tunataka mabadiliko lakini inaweza kuwa ya amani au ya vita lakini itakuwa mabadiliko sababu watu hawataki kuishi vile masiha iko wale wanalalamika ni 10% wale ambao wameshiba. Nataka kusema hiyo job one person I think we should put it someone ame-propose lakini ilikuweko sana watu walisema lakini nimewambia hata mkiwa na lalamika tunafanya kazi mpaka saa saba za usiku na saa tisa za usiku lakini ni na kazi moja na mshahara moja lakini nilipokuwa university hali ya waalimu unaenda unafanya examination council kidogo unafunza U.S.I.U kidogo unafanya little lecturing mwishowe unakuwa tu mtu ambaye amechoka na hata hana …(inaudible)… saa zingine hata una timetable yako una halafu unakuja ata unaenda kulima nyumbani. Vitu kama hivyo. Sasa hiyo kitu ya one person one job lakini ni mzee alisema wakulima wawe wakulima na watu wa office wawe watu wa office hiyo ni kitu muhimu. Mtu awe na kazi moja a concentrate okay …(inaudible)…

**Joseph Otieno:** Jina langu ni Joseph Otieno Pesa. Napendekeza ya kwamba baada ya kutengeneza final document ya katiba yetu ya Kenya ningependekeza ya kwamba mtengeneze katiba na iwe katika DIDCC iwe kwa mta wale ambao wanaweza kununua there na copies zetu ili tuweze kujua katiba yetu inasema namna gani. Wengine wetu tulipata shida sababu hatukuwa tunaelewa ya kwamba katiba ya Kenya inasema nini lakini kila tutawezesha kununua copies tuwe nazo tutakua katiba yetu asante.

**Com. Adagala:** Hata nikuletea hiyo katiba ya Kenya huwezi kusoma ni kingereza kigumu sana. Ni kingereza kali chenyewe cha Queen's council ile ya ndani kabisa. Pia ikipitishwa nafikiri inawza kuwa hivyo watu wajisomee wenyewe kwa lugha yote na mjitayarishe mtu atafsiri kwa Kinyore, Kimaragoli au msikizane Kiluyha ni Kiluyha gani mtaelewa iwe *indagano* watu waelewa nidyo pia lugha yetu itapata nguvu. Ulisema iwe kwa? Kwa mahali inaweza kununua.

**Otieno:** Ya kama DIDCC tuko na library …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Hata kwa bookshop ziweko ziwe na nafuu. Kenya tutatengeneza mwishowe iwe pocket constitution iko wapi. Leo ilikuwa hiyo the late Ombaka alikuwa na public law institute na itatengeneza hii. Hii ni pocket constitution. South Africa ukianza kumnyanyasa mtoto wa hiyo street boy au girl anatoa kwa mfuko anakuambia this is the constitution it will protect me. Unaninyanyasa mimi ni mtoto anatoa anakuonyesha sasa inafaa iwe ni kitu tunatembea kama kale kabibilia kengine kadogo.

**Interjection:** …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Well, itakuweko sijui kama itakuwa free au la, lakini pengine mwanzo itakuwa halafu pengine lakini hiyo ilikuwa kwa mapendekezo lakini kitu kidogo kama hako hii ni ya zamani. I want to close anybody who wants to speak.

**Arthur Kadedi:** Majina yangu ni Arthur Kadedi. Nashukuru hii tume ya kurekebisha katiba na je hiyo ndiyo mwisho wa nyinyi kutembelea Vihiga. Yaani hawa wanatoa maoni yao pamoja na nyinyi je mtafikiria hawa watu wamesaidia tupate kitu kidogo .

**Com. Adagala:** Okay, ni kama utalipa kuzaa. Utanilipa nikizaa mtoto wako. Huko Ujerumani wanawake wanalipwa ndiyo wanakubali mimba kwa sababu watu wamefika below zero population growth. Sasa nakuuliza tu, nikizaa mtoto wangu utanilipa? Mambo yako kwa katiba hii itakufaidisha hata kuliko kitu kidogo tunataka kutoka kwa mambo ya kitu kidogo tafadhali. Hatutaki handout watu wamekataa wanasema heri tupewe education system ya free. Ukipata watoto hulipi, angalia huku hulipi karo, no school fees itafurahi nakuuliza rudi hapa kitu kidogo ndiyo kitu tunataka tuwe kabisa na bunduki unasikia isitaje kitu kidogo mbele ya tume tena pengine mbele ya mahakam hao wanachukua hatuko kwa hiyo biashara unasikia lakini tutakuletea manufaa ukienda hospiitali uende utibiwe vile ulikuwa zamani hao matajriri walipe ushuru wewe upate huduma unasikia basi mambo ya kitu kidogo *ritswe* (laughing).

**Thomas Kipkenda:** Kwa majina ni Thomas Kipkenda Orunze nikiunga maoni hii tume ya leo hivi kutuongoza vyema mpaka kufikia saa ya sasa hivi. Na kwa ufupi ningependelea kwa u-president vijana wachukue u-president kwa sababu nikiangalia sana sana wazee nao wengin wameangalia

**Com. Adagala:** Ulikuwa hapa umri ya mbunge nikuanzia miaka gani?

**Kipkenda:** Ishirini na mbili

**Audience:** ah …(inaudible)…

**Com. Adagala:** Inafaa niwape mtihani nyinyi. Mmeketi tu hapa 21 yrs old, members of parliament, songa member of parliament upate ujuzi ufike miaka fulani umri fulani upande ufike kwa u-president sijui kwa wewe youth ni miaka ngapi ambaye anaweza kukua president wengine walitoa maoni yao ulikuwa hapa wakati ule muamuke na kwamba tunaenda mahali kwingine kanisa inaja na nje kwa madirisha hapa hamjaamka mpike kanisa kubwa kuliko hata hii faith zile za catholic watu wanajaa na nje kwa madirisha ndiyo tuna hii loud speaker ili wasikie haya MP 21years is that okay. Mtu wa national council 35 kwanza president ni 35 kumaliza ni 70 iwe inasimama unamaliza hiyo 75 mwisho okay hiyo inataosheka au unataka tuweke 18 unaona tumefikiria haya.

**Kipkenda:** Sasa kitu kimoja cha kuzingatia kwa sababu mimi ni mkristo asiwe mlevi hata pingamizi napinga shirikwe pombe upigwe marufuku Kenya.

**Com. Adagala:** Kwanza, ngoja ukisema asiwe mlevi basi atakuwa mwislamu kwa sababu wakristo wanasema ni wakristo na wanakunywa, waislamu hawakunywi. Sasa ukisema asiwe mlevi kweli nakwambia unasikia. Wakristo wamekataa kusimamia

mambo yao hata hapa kuna kitu kinaitwa kuna repot watu walitaka christian triburnal ili wakristo waishi na sheria ya kikristo ile ya Musa na ile na Yesu na ya Paul naishi nayo unasikia haya lakini hatuna mtu anasema tu anaenda kanisa halafu anafanya yake ufisadi, anatukana wengine anaishi vile anataka kuishi, anakunywa pombe na anasema ni mkristo. Office ya wanasheria ni watu walisema lakini we don't have it here kwa sababu wenyewe hawakupigania sana hata watu wa kanisa hawapiganii sana hiyo tuwe na sheria ya kikristo ya kuishi waiislamu wametushinda sana. Kuna iko kwa katiba …(inaudible)…

**Kipkenda:** Kwa hivyo nimekupongeza sana hata asante sana kwa vile tena mapata gati kama hii kwenda kuhutubia wengine asante sana.

**Com. Adagala:** …(inaudible)… utuhutubia na usome na wengine haya tumemaliza tunataka kumshukuru nilikuwa sijawajulisha. Hii team yetu kule kuna wanaita verbatim reporter anaandika kila neno vile mnasema ndiyo mnaona tu-switch kutoka kwa Kiluyha tukaenda kwa Kiswahili na Kingereza kila neno yeye alikuwa anafanya kwa bunge kila neneo inaandikwa hapo inaitwa verbatim na maripoti yetu na popular meeting zetu zote the plenary zinaandikwa hivyo huwezi kusema sikusema wanaenda wanasema record inasema aje wanamwita Patricia Mwangi yeye tulikuwa na yeye shule miaka ya ukoloni bado sana alikuwa mkubwa wangu alikuwa classmate na Margaret Sabwa. Si mnamjua Margaret Sabwa? Walikuwa waje sasa mimi after commission najua mkitaka kulia dada yangu mkubwa. Na huyu ni Vincent Watako Muwanga niliwaambia mnipe Mluyha niende naye sitaki hii mambo ya kuwa kuna shida nyingi lakini kunaonekana kiwanga pia hatuingizani vizuri lakini hii mambo yote ni ya utamaduni wetu. Halafu district co-ordinator wenu ako hapa kamati iko hapa mmeangazwa pia sehemu ingine na tume inaitwa national constitutional conference wenyewe walichaguliwa wako hapa simameni wakati ni wafrika nani mwingine …(inaudible)…

**Agnes:** Sasa vile mnavyojua tuna national constitutional conference, ambayo ni sehemu ya hii proces ya kurekebisha katiba na ni lazima kila district itowe representatives wake ambao watawakilisha kwa hiyo NCC. Sasa tulikuwa na nominations ambazo zilikuwa published na magazeti, radio na ikawa tutakuwa na watu watachukua forms wa submit their nomination papers halafu eventually tukawa na uchaguzi. Kwa huu uchaguzi tulitakikana tuwe na delegates wa kuwakilisha wanawake wa Vihiga district kwa NCC na vile tulifanya uchaguzi tulipata Mrs. Rebecca Avelia ambaye atawakilisha wanawake kutoka Vihiga district.

**Rebecca Avelia:** Majina ni vile mmesikia Rebecca Avelia nitawakilisha wanawake kutoka Vihiga.

**Agnes:** Mmesikia ikiwa mko na maoni mengine ambayo mngependa yawekwe hapa ama kuna kitu ambacho mnataka kubadilishwa tafadhali mlete maoni yenu kwangu mimi hata kwa hawa halafu zitawakilishwa huko. Na pia tulitakikana tuwe na mwakilishaji civic leader although haikuwa ni lazima walisema tunaweza kuwa na at least one person ambaye ni councillor an vile tulifanya uchaguzi councillor Caleb Juma na councillor Calen Nyanji walipigana ana kwa ana na councillor Juma akawa mshindi akachukuwa hiyo slot ya kuakilisha councillors.

**Counc. Caleb Juma:** Asante sana hamjambo wote. Nafikiri yangu ni kutoa shukrani kwa siku ya leo na commissioner na mwenzake yule ambaye anachukua record hapa. Nafikiri kwamba yale ambayo yamebaki kama una kitu ambacho unafikiri

ukisoma hiyo gazeti ile ambayo mko na …(inaudible)… inaweza kuleta kwanini nifikie pale nitaongeza kwa yale tutaenda vile vile asante sana. mimi nitaakilisha …(inaudible)… ukileta kwa county council hapa Vihiga uandike kawa jina langu Caleb Juma nitapokea weka tu wacha tu kwa ofisi hapo county council nitayapokea kwa sababu iko askari hapo full time asanteni.

**Agnes:** Halafu tulikuwa na open seat ambayo ingegombewa na mwanamke au mwanaume na tulikuwa na wagombea karibu ishirini wale wakupigania hiyo kiti na mshindi wa hiyo slot alikuwa bwana Charles Ohare ambaye nidyo huyu na atatuakilisha karibu Mr. Ohare usalimie wananchi.

**Charles Ohare:** Commissioner na wananchi hamjambo? Mimi naitwa Edward Charles Ohare kutoka Bunyore. Mimi ni mfanyi biashara, retired civil servant as the district commissioner. Nafurahi sana kwa kuchaguliwa ili uchukue maoni yenu kwenda nayo kwa national conference na kama mna neno mtueleze na yeye atatoka Tiriki, hapo South Maragoli na mimi natoka Bunyore. We are spotted around district yetu vizuri kama kuna jambo mniletee tutwapelekea tutakwenda kule kuwakilisha na I want to assure you that we shall wakilisha nyinyi effectively. Asanteni.

**Agnes:** Okay asante Mr. Ohare. Ningependa kuwahimiza delegates wetu ambao watatu-represent muendelee kujifunza vile tuko na commissioners hapa muweze kutakilisha kwa njia ambayo itakuwa mzuri. Asanteni.

**Com. Adagala:** Sasa nyinyi mjiunge na committees ya 3C's ili nijue na tena ma-governor kidogo mwafanye wafanye kazi zaidi kwa sababu huko itakuwa vita na mumefurahi Vihiga watu ambao wanaweza kupambana huko itakuwa vita. Nimesema ni market lakini pia itakuwa mtu anashika jambo la kwao hawezi kumsongesha na mimefurahi. Hawa watu nawajua ni wetu mashuhuri ni watu ambao wataweza kufanya kazi hiyo vizuri. Sasa jiungeni na hiyo halafu kuna seminar inakuja halafu mtakuja mtaenda kwa NCC ambayo itakuwa Bomas of Kenya. Nataka kuwaeleza watu wengi walilamika chief, councillor yuko mmoja ako kwa location, location hiyo ndiyo ward hii ni nini. Watu wanatuambia tumeongeza bei tumepunguza bei ya vitu cost of things kwa sababu sasa kwa hiyo location tutakuwa na mwakilishi mmoja sio mbili ilikuwa chini sivyo chief na councillor wengine wanasema tu ndiyo afanye kazi na wengine wanasema councillor ndiyo wanafanya kazi councillor ndivyo anafanya kazi sasa tumefanya chief atakuwa electable atapeta chief lakini kwa njia ya councillor.

Okay hayo kwa hivyo nimefurahi sana hiki kilikuwa kikao cha tume ya kurekebisha katiba hapa Kidundu tumefurahi kupitiia mara ya pili mnaona leo niko peke yangu kutoka kwa tume lakini tulipakuwa hapa tulikuwa watatu sasa hii ni kazi ya kufundisha sasa tukasema tufanye haraka mtu mmoja kila mahali. Nilitaka kusema kwa district nimefurahi kwa sababu mimi nimetoka Sabatia na nilisema wakichagua mtu mwingine kwenda kwa NCC kutoka Sabatia wengine unatakaje na sikuambia mtu lakini kwa busara yenu mumeweka Vihiga, Hamisi, Emuhaya, Situko saswa na nimefurahi hapo kwa sababu watu wakifanya vitu kwa njia ya ukweli siyo ya godfather watu wengine walisafiri mpaka Nairobi wanatafuta commissioners ninataka kuwa kwa hiyo kamati mtu amemwambia ata uchaguzi unaendelea nyumbani unafanya nini mpaka Mombasa tulipokuwa tunatengeneza katiba *sololа mang'ana kago golia mpala ewenala*. Haya *khunyanzi ndolo chandanyanzia Vihiga kupe na pandu pagangana anang'ana kali maripoti getu kapeha igilu kwa njila yenye kupe na pandu pangangana amang'ana* isipokuwa unajua tumekuwa watu wa serikali *ndi* na tumekaa kwa hiyo sasa na sasa serikali hii inafikiria kwanza ni wananchi ndiyo serikali na

hawa wengine wanapata nguvu na nguzo kutoka kwa wananchi ndiyo inaenda juu. Haya Sabatia tumefurahi ingekuwa bora mngekubali mungekuwa Mbale kwa sababu mimi huko ni Vihiga lakini nilisema si Vihiga constituency hapa ndiyo tungekuwa na watu wengi sana lakini kweli ni cosmopolitan hata Wajaluo wameingia hata Wanandi sasa hii ni yenu naelewa hapo. Kitu kingine ni nini? Natachukua maoni yenu nimeinasa hapa kama hauna hii watu wote wako nayo.

Kama uko upande wa ma-judges au upande wa mtu mwingine anapinga katiba usivae, okay hiyo ni ya kuonyesha wazi kila siku uweke vizuri halafu unaweka tena. Kesho wakili woe watasusia mahakama hawataenda mahakamani kwa sababu ma-judge wamefanya kitu kibaya sana kupinga katiba. Hao ndio wanafaa walinde na wao ndiyo wanapinga kwa sababu ya self interests kwa sababu ya ubinafsi wanafikira nimetajirika sana watakuja kuniuliza na nini watakuuliza tu mshahara yako ni hii tuambie vile umepata hii nyumba na ile plot na magari saba hivi ya mercedes hiyo ndivyo watauliza hukana kitu kikuwa na utasema na hii nilipata kwa Pattni tulipokuwa naye na hii watu wengine waliua mtu mwingine na nikamtoa ndiyo akanipa.

Watu wamefanya hata kazi ya Pattni, wanasema kwa mwezi moja maisha yao inabadilika kwa sababu anakuja tu anakupea tu pesa, anakuja na submission’s imeshaandikwa ukimuuliza nani ameandika hii anasema judge aliandika wewe soma tu. Sasa wakili wengine walikataa wakasema hiyo ni nini wanakataa halafu anaondoa anachukua mwingine anampa pesa. Soma hii pia amekubali anapata pesa ingine. So, we have a lot of problems. What we are doing ni ile ambayo constitution ina common good for the greatest number of people sasa kama watu 90% ni masikini tufanye aje tutakeleza yao. Tajiri na masikini hata kwa kitu chochote hawawezi kusikizana ni kama mtu ameshiba na mtu ana njaa au mtu mgonjwa na mtu anakwambia na kwa nini unalala siuamuke kwa sababu yeye ako mzima.

Haya pengine nimesahau mengine mambo ya wanawake ni ule tunasema cross cutting iwe inaanzilia kwa preamble hiyo inazungumzia equality haukuwa hapa. I was very sad, Avelia very sad that you were not here, I didn’t find you here kwa sababu tumezungumzia mambo tuko 1/3 way through mnaanza kuja si kazi ya aina hiyo na tena awambie kule kwingine tunaenda watu na kamati hawa watumishi wawe hapo na mbunge. Mambo ya wanawake ni cross cutting kutoka kwa equality, kwnda kwa citizenship, basic right, shamba, devolution kwenda kwa kila kitu wanawake wako hapo na si bunge peke wako hapo sasa ukae chonjo mjue namshawishi hawa wanaume to believe in you they love you but he need to believe in you that you are also human beings. You need to convince them that, because actually what it is in the culture you are not a human being. *Muda epukuango hao awa ndiza na mkele hano omundu mwene apola no. apapola omundu na mkele pengenda gunzeili* hiyo ni nini. Si binadamu kwa hivyo kila mtu ni binadamu *muhanza* chukua hiyo yote mjifunze msome kabisa soma hiyo kabisa inatakikana korti chini na wakili ujue ni nini inaendelea. Tutawacha vitu hapa vichache mmechukua vingi lakini tutaongeza hii na kwa hiyo. Hiyo ni ya kamati na district co-ordinator something to read lakini musome magazeti ya katiba si nimewaambia.

Kina baba mtasumbuka ndani ya nyumba kwa sababu mtakuwa mnatarajia vitu vitaneda hini na hivi na watu bado wako kwa ile 19th and 20th century. Sisi tuko kwa 21st century tunaenda mbele. Yule mtu anataka kuenda tuandamane, yule anataka kubaki abaki. Lakini sisi tunataka maisha mpya. Kenya mpya by this time next year Kenya will be a different country. Hata nitakuwa nikisema hayo, wazee hukumbukka vijana watakuwa kwa wazee hukumuka kwa sababu ni mambo ya zamani mnaelewa nini

ingine mnataka niseme. Tumeendelea na kazi yetu vizuri msikuwe na hofu mkisema tukigombana nje tunaoenekana tukigombana kwa sababu tuko watu wa aina tofauti yote ya Kenya hapo tofauti zote ziko hapo za siasa za tribal za asilia wanawake, wanaume walemavu wengine wakili na hivi sasa lazima kuwe na msukusuko wapi. Lakini sisi wenyewe tunajua njia tunaelewa na lazima tutimize mambo yenu. Nimefurahi tumeketi hapa tulianza kama saa nne na nusu hivi mpaka sasa saa kumi na mbili nimefurahi tulianza na maombi ya mwisho tutauliza kamati tunataka hii kamati iwe active na tunataka wawe na mkutano kama nne, tano hivi kabla nasea hadharani, muwafuate mumeona kule wanatoka na hawakua kumi wako seven nafikiri wale niliona hapa wengine wamelalia masikio.

Mfanye, mshirikiane ili mjue msome mambo msikize habari kwa sababu ya tume na mambo ya katiba na pia mazungumzo na wabunge wenu wajue tuna haja hayo ni maisha wananchi watu wengine ni matajiri na wana vitu vingi wanaenda kuishi nchi ingine au nini. Lakini hao wako hapa ndiyo tung’ang’ane nao. Nisipotee kwa mambo ya siasa au katiba niliona sehemu a siasa ya elections kwa hii chapter moja na nijue hiyo, hiyo ndiyo sehemu yake ya maisha. Maisha mengine yanaendelea, wengine mmeiomboleza kwa kifo cha baba kweli tulihuzunika kwa sababu alikuwa anapona baba Solomon Adagala. Alikuwa anapona lakini naona ni kama ilikuwa Mungu alimchukua pengine aliona akiishi zaidi dunia itamharibu akachukua mwenyewe alikuwa ameomba Mungu alikuwa anamuomba kuuliza kusamehewa na kujitokeza hivi vitu kama hivyo usiku na mchana na alikuwa na furaha alipenda hata kwa kitanda alikuwa amelala tu kama amejitayarisha mwenyewe na hakuwa na uchungu hapo lakini tukijaribu lakini, binadamu tu ni mtu wa siku chache tu na tumefurahi mlitusomesha vizuri alikuwa yatima *yali amupisandu* lakini mtu alimpenda inaoenakana na *pape ye yali yapola ndi siku yakulikunzi* ndio akaenda *emasepo na bilukiayo* lakini mwishowe yeye ndiye alikuwa mtoto wa Ngaiwa na mwisho kufa na wengine walikufa zamani sasa hiyo alikuwa kifo ndiye alikufa mwisho na tulifurahi, tuliona mkono wa Mungu uwa maisha yake na tulimjua vizuri alikuwa anakuja huku alipokuwa kwa Vihiga Friends namjua vizuri.

Sio mtu ambaye mimi naweza kumueleza hata mwenziwe kunieleza zaidi kuliko mimi naweza kueleza tulipenda lakini inaonekana Mungu alimpenda zaidi na alituachia jina nzuri tunafurahi alitulinda kama baba akatupa ile nyumba boma ambayo yeye hakuwa nayo sasa ni kama alitupenda zaidi, kuliko alijipenda. Na mwishowe hata alijua hivi mambo ya katiba hata akaja huko Vokoli lakini hakuwa na nguvu ya kuzungumza akaketi tu kidogo tulimbeba tu kwa gari hakuwa anatembea akaketi akasikiliza kidogo akachoka akaenda nyumbani, lakini alisema kitu kimoja anaona mayatima wanasumbuka sana na pia kuna mambo ya mayatima hapo.

Pili, akasema wazee wakongwe wanasumbuka sana kwa sababu hawana namna nafikiri alikuwa anajiona hapo hata kwa hiyo ya mayatima alikuwa anajiona sasa hata waliweza katiba lakini pia kanisa ya Friends nilizungumza hiyo mambo international bomb na hapa pia nafikiri vile tunaweza kusaidia mayatima na pia wazee wakongwe kweli niliona mwishowe tulimwandika nurse na kumlinda na mkaona pengine hapo waweze kuwa kitu kuwe na watu ambao wanahudumia wanawatembelea wazee wakongwe kwa sababu kwa njia yenywe ni kama mgonjwa kwa sababu akili pia waanza kupotea na mtoto wangu akamwabia *guka ako* fine kwa sababu ugongo ni kama uzi sasa ukizeeka unakatika *pioroi* siyo hivyo hivyo sasa vile anakumbuka ni vya zamani ndivyo viko sana hata kitu kinatendeka hakumbuki kitu lakini kwa Maragoli tunasema alomaloma na *pagunza sikape*

ndio na siyo kuzungumza na *pagunza* anazungumza mambo ya zamani anakua mtu wa historia sasa asante wale wazee bado mko muishi, mudumu kwa sababu tunataka tuwe na nyinyi zaidi muone ibadilike iendelee vizuri. Asanteni, Mungu awabariki.

Asante kwa kutuombea tuliweka kwa ripoti yetu watu wote wanatuombea na tukisema kweli kazi yetu ilikuwa hiyo ripoit hii ukisoma tulikuwa tunafika mahali halafu vitu vimekua vigumu hata tukilingina huwezi kuwa hata kama huyu kijana alisema hakuona vile hii kazi itakamilika halafu mwangaza unakuja na vitu vinaendelea tu mbele na ni hiyo kuomba tu hata sisi ndani tulikuwa tunaomba isipokuwa mzee Ghai haamini Mungu lakini nafikiri ameanza kuona kuna kitu zaidi ya binadamu kuna watu wengine wanakaa hivyo sio wanadharau Mungu au nini wameishi tu binadamu ni binadamu hakuna kitu kingine mbele wanaitwa atrocities. Sasa mumuombe yeye pia aje karibu sivyo lakini alikubali tuweke Mungu aibariki Kenya kwa katiba. Asanteni.

**Agnes:** Haya asante sana commissioner na wenzako ambao ulikuja nao kutufundisha hii kazi ya draft ambayo tumetengenezwa. Nigependa kusema asante sana kwa sababu tangu wakati ule commissioner alikaa hapa hivi ingawa anavumilia hajisikii vizuri lakini amekuwa mvumilivu sana ametufundisha bila kuchoka mpaka wakati huu. Halafu kuna kitu ambacho ningependa kugusia kwa sababu pengine vile nitapatia chairman fursa ya kuongea pia anaweza akasahau. Ningependa sana kumjulisha commissioner Adagala kwamba, tangu wakati ule ambao commission iliweza kutoa hii draft constitution na ikawa published kwa newspapers mimi kwa ofisi yangu nimeona wananchi wa Vihiga district kwa wingi sana wakija wakisema congratulations, maoni yetu ile tulipeana ndiyo ambayo imeonekana kwa draft constitution na vile tuliona some lawyers na later on judges wakienda kwa court wajue commission imeona wananchi wa Vihiga district wakija wakisema tuko nyuma ya Professor. Kamati yake na wajulishe ya kwamba wasiogope si tutawaunga mkono na tuta-support upto the very end. Sasa commissioners ukienda Nairobi ujue watu wa Vihiga district are firmly behind the commission and they will support you to the very end sana kabla nimalize nitamwita chairman wa Vihiga consituency committee afunge huu mkutano. Asanteni.

**Com. Adagala:** …(inaudible)… ambaye imetoka kwa district yako na kuonyesha juu ya …(inaudible)… na iwe watu wanaweza …(inaudible)… mara waripoti nyingi pengine maili tatu hivi ndiyo iko a little bit bigger …(inaudible)… watu wawe …(inaudible)… (clapping).

**Lugadiru:** Nitachukua nafasi hii, si nafasi ya kunena lakini nafasi ya kumshukuru commissioner Kavetsa kwa kazi ngumu ambayo amefanya siku ya leo. Na mimi mwenyewe sikufikiria itakuwa vile imekuwa na pia ningependa shukrani ingine iende kwa team yake ambayo wamekaa hapa kwa muda mrefu kutoka asubuhi nasema asante sana. Na tena nachukua nafasi hii ya kushukuru nyinyi nyote wananchi ambao mlichukua nafasi ya kufika kwa mambo haya ambayo yataweza kubadilisha mwenendo katika nchi yetu ya Kenya special shukrani ningependa ni same tu waili sisi sote tumefanya vizuri lakini kwa nyinyi nitasema special shukrani kwa kiongozi Bulira na Kaiga wazee hao wamekaa tangu asubuhi na wangali ana sisi na haya yanaonyesha uongozi ulio mwema kiongozi lazima uone ya kwamba unajitahidi hata ukiwa kwa shida ya kukaa unakaa mpaka mwisho.

Mimi nasema asante sana kwa nyinyi nyote kwa kuja hapa. Wale ambao wamepata nafasi ile ambavyo wataakilisha sisi Nairobi tena mimi nasema asante na nyinyi mukae na watu wenu karibu ili wampatie maoni ya kuongezea ili wakati mtaenda Nairobi

mfanye vizuri hata councillors wetu ambao hawako hapa, tuna deputy mayor hapa, ambaye ni member wa kamati ninasema asante sana. Kwa kumaliza nasema hatuna kitu ambacho tutapatia commissioner na team yake ni tutengeneze tu mikono yetu na commissioner uende useme Vihiga constituency inaunga commissioner Ghai na timu yake mkono kikamilifu. Waendelee na kazi na hakuna kitu ambacho kinaweza kuogopa. Wacha wale watu waseme mambo yao lakini tunajua wananchi wanaendelea mbele. Ni asante.

**Com. Adagala:** Ripoti ya kwanza tulipata tulipoweka ripoti yetu kwa gazeti tarehe 27 September, ile ripoti tulipata ya kwanza ya district co-ordinator ilikuwa ya Vihiga district na nikasema kwa plenary vile walituambia watu wengi vile wanazungumza wanatuunga mkono na tulikuwa tumepitia kidogo tulikuwa tumechoka na mahakama wanatupinga wote watu walisema vizuri eh ni vizuri sana hata Ghai akasema oh really! Na nywele yake ikafanya hivi na akawa na furaha na wa pili alikuwa wa Lugari sasa inaonekana tuko chap chapa. Nimefurahi kwa hiyo.

**Speaker:** *Mwakahulila ni Vihiga hino ni patanya Prof. Ghai umokono ku katiba zinzegindi kuduka kunyole …(inaudible)… makano kusingiri …(inaudible)… (clapping)….* Tutaomba mzee mmoja atumalizie na maombi na kamati mtabakia nyuma kidogo tuzungumzie jambo kamati ya Vihiga constituency mzee karibu.

**Lugadiru:** Mimi ni Manasseh Misee Lugadiru chairman wa Vihiga committee.

**Pastor Reiga:** Nafikiri tutamshukuru Mungu. Mimi kwa majina kama nilivyosema ni Pastor Reiga haya tuombe.

Asante mwenyezi Mungu tumeinama mbele yako kwa heshima tukiwa na imani kwa yote ambayo tumeyasikia umetuongoza tangu tuanze mkutano huu na umetulinda vizuri na yote ambayo tumezungumza na viongozi wetu ambao wanatengeneza. Umetuongoza Baba, tuna furaha kubwa kwa sababu ya upendo wako umetulinda mpaka saa hii na sasa hivi tunataka kutawanyikana kwenda mahali tulikotoka na hawa viongozi wetu wa katiba yetu ya Kenya ninawaweka mbele yako Baba mwenyezi mungu. Waongoze yale ambayo wanatumia, maneno yale ambayo wanatumia, maneno yale yote wanasema uwanyang'anye yao uwape yako na hii itajenga nchi yetu.

Sasa hapa tutatawanyika tu kwa mwili Baba mioyo yetu iwe kitu kimoja tuwe pamoja mkubwa wetu wa commissioner ambaye amekuwa hapa akiwa nyumbani Nairobi, Mombasa, wapi roho yake na roho zetu ziwe pamoja na tuwe kwa laini ya mbele kuongoza namna ya katiba ya nchi yetu ya Kenya itakavyokuwa. Wakati wanaondoka uwaongoze uwe mbele na wakufuate ukiwalinda na kuwatunza vizuri kwa sababu, ukiwa pamoja nao hakuna kibaya chochote. Kwa hivyo Baba wameenda kwa magari na wewe mwenyewe waongoze na wafike salama na kila mtu aliye hapa vile vile afike nyumbani kwake salama mpaka tena wakati tutakapo kutana lakini hiii ni shangwe kubwa tunakupa heshima kubwa kwa yote ambayo umetutendea wape uzima wa mili yao. Wape uzima wa mioyo yao na wafanye kazi yako vile vile ni kazi ya nchi yetu hii lakini wanakufanyia kazi wape afya nzuri na waendelee vizuri mpaka tutakavyokutana tena tukiwa na furaha kuzidi hii. Haya Baba naweka mbele yako katika jina la Yesu mkombozi wetu. Amen.

**Audience:** Amen.

**Lugadiru:** Basi na mfike salama.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&